

YEHOVA-YIRE

 Asanteni. [Ndugu Slater anazungumza—Mh.] Asante. Asante, Ndugu. Asante, Ndugu Slater. Bwana akubariki.

² Mnaweza kuketi. Ungewezaje kukataa makaribisho kama hayo? Hakika nakushukuru sana kwa makaribisho hayo mazuri, Ndugu Slater. Nami najua unanena katika mioyo ya hao ndugu wengine, uliposema hivyo, shirika, na wote wanaohusika, na kwa wasikilizaji. Asanteni, sana.

³ Mnajua, daima unaweza kujisikia kukaribishwa zaidi kama mtu fulani akikwambia jambo fulani. Mtu fulani alisema wakati mmoja, nilikuwa nimehubiri na nilikuwa nikitoka, mtu fulani akasema, “Ndugu Branham, huo ulikuwa mzuri kweli.”

⁴ Kulikuwa na mhudumu mwingine aliyekuwa akitembea karibu nami, akasema, “Nina furaha watu hawajivuni kwa ajili yangu.” Akasema, “Sitaki wajivune kwa ajili yangu.”

Nikasema, “Vema,” nikasema, “Ninaamini.” Nikasema, “Mimi . . .” Nikasema, “Na—napenda hilo.”

Naye akasema, “Vema, hakika sitaki waseme . . .”

⁵ Nikasema, “Tofauti moja tu kati yangu na wewe: mimi ninasema kweli, nawe husemi kweli, hivyo tu.” Hakika.

⁶ Baba alikuwa akinifanya nifanye kazi kwa bidii mara mbili kuliko vile ningefanya kwa sababu aliniambia nilikuwa nikifanya kazi nzuri. Kwa hiyo, sisi sote tunapenda hilo, tunapenda kuambiwa. Na—na halafu ninathamini ukosoaji mzuri, wa kirafiki wakati mtu anaposema, “Sasa, ulifanya kosa hapo, ulifanya jambo fulani.” Ndipo ninajua, nitajaribu kurekebisha hilo. Mnaona? Sikuzote ninavutiwa na ukosoaji, nanyi je? wakati ukiwa sawa. Uone kama una—kama unakosea, hutaki kufanya hivyo. Mimi . . .

⁷ Mtu fulani alisema, “Vema, ni—ningelikwambia, lakini mi—mimi . . .” Vema, hakika, kama wewe ni ndugu yangu, unapaswa kuniambia, nataka kujua hilo.

⁸ Mtu yeyote anayetaka kwenda Indiana pamoja nami? Nilimpigia mke wangu simu dakika chache zilizopita, na kuna inchi kumi za theluji, imeganda kila mahali, barabara zote zimefungwa, madaraja yamefungwa, bali hakika mnakaribishwa kwenda pamoja nami. Itayeyuka katika siku chache, msimu umechelewa sana kwake kukaa muda mrefu sana.

⁹ Kwa hiyo tunaondoka mara baada ya ibada alasiri ya leo. Tujaribu kufika nyumbani kwa wakati unaofaa wa karibu kupitia mlango mmoja na kutokea mwingine, tupate siku chache za kukaa. Kisha twende huko Virginia, yapata maili mia tisa

kutoka nyumbani tena, na huko chini kwenye pwani ya bahari pamoja na kituo kikubwa cha baharini, ama, kituo cha jeshi la wanamaji, na kadhalika. Tunashuka kwenda kule kuwaleteta Injili, kulichukua kundi hilo la wahudumu, na kuweka wavu wetu pamoja nao, tuone kama tunaweza kuwashika watu fulani mahali fulani.

¹⁰ Halafu basi kutoka huko turudi kisha tuingie Ohio, na halafu kutoka huko tuingie Bloomington, Illinois, kisha Chicago katika Shule ya Upili ya Lane Tech ambako kwa kawaida tunakutana huko. Ukumbi mkubwa mzuri wa mikutano, unaoketi yapata elfu nne ama elfu tano nasi tunaweza... Huo utadhaminiwa na Wafanyabiashara Wakristo na tawi la Chicago, hiyo itakuwa juma la mwisho katika Aprili. Halafu mnamo Mei, niko British Columbia, na huko juu Dawson Creek, na Grande Prairie, Fort Saint John, kuendelea na kuendelea, mnajua jinsi iendavyo.

¹¹ Kwa hiyo, ninataka kuwaomba jambo moja, nataka mnifanyie fadhili. Mtafanya hivyo? Ninii tu, wakati mnapoomba, nikumbukeni. Mtafanya hivyo? Ninapokuwa ng'ambo, na wachawi wamesimama pale, na nguvu za pepo kutoka kila upande, ninaweza kukumbuka nina marafiki wa kweli hapa ndani wanaoniomba, hilo litanifanya niwe jasiri kuondoka, nikijua ya kwamba mnanishikilia katika maombi. Ninathamini hilo.

¹² Ninataka kutoa shukrani zangu kwa shirika hili, wahudumu hawa wote wanaodhamini. Nilikula kiamshakinywa pamoja na wengine hivi majuzi asubuhi, niliwaambia, nami ninaamini wameongeza wengine tangu wakati huo, kwa hiyo bila shaka na—nathamini ushirikiano wenu mzuri. Madhehebu mbalimbali yanaingia tu, yakivunja, sisi ni ndugu tu, na hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Ninatumaini ya kwamba hilo kamwe, kamwe halitaondoka mahali hapo, sikuzote tutakaa hivyo, sisi ni ndugu.

¹³ Na kwa kufanya hivyo, nafikiri nimepewa na Mungu, mojawapo ya miamsho midogo mizuri sana ambayo nimekuwa nayo kwa miaka mingi, papa hapa. Sijawahi kuona watu wakimwonea Mungu njaa zaidi, kuliko nilivyoona papa hapa, sijaona mahali popote Marekani, kuliko ilivyo moja kwa moja katika bonde hili.

¹⁴ Nilienda kwenye maeneo ya biashara, maskini msichana Mkatoliki alikuwa anatandika kitanda katika hoteli niliyokuwa nikiishi, naye alisema aliishi karibu na Wapentekoste fulani, akasema, "Je, wewe ni Mpentekoste?"

Nikasema, "Naam."

Akasema, "Mimi ni Mkatoliki."

Nikasema, "Nami vivyo hivyo, pia."

Naye akasema, “Unawezaje kuwa Mkatoliki na Mpentekoste wakati uo huo?”

¹⁵ Nikasema, “Vema, angalia, hivi Biblia ya Katoliki haininii...? Hivi—hivi hamsemi, ninyi Wakatoliki hamsemi ya kwamba Biblia ni historia ya kanisa Katoliki la mwanzoni?”

Akasema, “Naam.”

“Ati Yesu Kristo alianzisha kanisa Katoliki?”

“Naam, bwana.”

“Ati na wanafunzi wote walikuwa Wakatoliki?”

“Uh-huh.”

“Na waliandika Biblia?”

“Uh-huh.”

¹⁶ Nikasema, “Basi mimi ni Mkatoliki wa mtindo wa kale, ninaamini yale Biblia isemayo, unaona.” Kama hayo yalikuwa ndiyo mafundisho ya kanisa Katoliki la mwanzoni basi mimi ni Mkatoliki, mnaona, si Katoliki ya aina hii mpya, ile Katoliki ya mtindo wa kale, mnaona, ile ambayo Yesu alianzisha.

¹⁷ Na jambo lingine neno—neno *katoliki* linamaanisha “ulimwenguni kote” kwa vyovyote vile. Kwa hiyo ni ninii tu...Kwa hiyo ninaamini katika dini ya ulimwengu mzima ambayo Yesu Kristo alianzisha kwenye Siku ya Pentekoste, kwa hiyo mimi ni Mpentekoste-Mkatoliki. Umewahi kuona mmoja hapo kabla? Na kwa hiyo hilo ni sawa kabisa.

¹⁸ Tunataka kushukuru kila mmoja wenu ninyi watu, ninii, kwa kulipa madeni. (Nadhani yote yalilipwa? Je, walichukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu? Yote yamelipwa. Nao wakachukua sadaka ya upendo? Sasa, kama hawajaichukua, wekeni hiyo sadaka ya upendo moja kwa moja humo, kuhakikisha yote yamelipwa.)

¹⁹ Hao ndugu wakasema tu...Kamwe sijui lolote kuhusu kitengo chake cha biashara, hao wengine wanashughulikia hilo. Ninajitolea tu kwa maombi, na kusoma Neno la Mungu, na kuona mahali Yeye ataniongoza, na yale ninayoweza kufanya wakati nikiwa katika hii jamii. Na kwa hiyo, walisema madeni yote yalilipwa, nao walikuwa wamechukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Sasa, haikuwabidi kufanya hivyo, mnaona, mradi tu mlilipa madeni, hilo tu ndilo linalohitajika.

²⁰ Lakini nitakuhakikishia, ndugu yangu, dada, ya kwamba—ya kwamba sehemu hiyo ya riziki yako, kwamba vizuri nijuavyo, pamoja na maarifa yote ambayo Mungu atanipa, itaenda kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, hiyo ni kweli. Na Mungu na awape thawabu kwa ajili ya msimamo huu wa kishujaa mliochukua, na—na kusaidea kuleta huduma hii bondeni humu, na awabariki mara mia moja.

²¹ Ilisema katika Maandiko, “Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hawa watoto Wangu walio wadogo sana,” huyo angekuwa ni mimi, “mmenitendea Mimi,” alisema Bwana Yesu. Na kwa hiyo, ninaomba ya kwamba Mungu atawabariki sana kwa ajili yake.

²² Na sasa, hiyo itatumiwa kwa ajili ya misheni za nchi za ng’ambo, kwenda kwenye huduma za kigeni na kuwahubiria watu ambao hawana hata senti moja. Huko, wamishenari wakihubiri Injili, bila viatu, hawana shati, wakihubiri Injili. Basi mngeweze kutarajia watu kama hao kudhamini mkutano? Wasingeweza kufanya hivyo. Ni nani angeweza... wanguweze kunigharamia kuja huko na kurudi? Lakini kumbukeni, pesa zenu mnazochanga zitatumika kwa kusudi hilo, kusaidia kuwaokoa watu hao ambao Yesu alikufa apate kuwaokoa.

²³ Nami ninajua ya kwamba zinapowekwa mikononi mwangu, mimi ndiye msimamizi wa hizo basi, tangu wakati huo na kuendelea, naye Mungu ataniwajibisha hilo kwenye Siku ya Hukumu, aniwajibishe, kwa hiyo ninataka kuwa msimamizi mzuri kufanya kila niwezacho.

²⁴ Na sasa, na kwa ajili ya maombi yenu mazuri na ushirikiano, kila usiku mahali hapa pamejaa, na watu wakarudishwa, nasi tunathamini hilo.

²⁵ Na ikiwa ni mapenzi ya Bwana, mimi hujaribu tu kwenda mahali anaponiongoza kwenda, mnaona, mahali tu ninapojisikia kuongozwa, basi ninaenda. Na halafu nikifanya hivyo, basi ninapokabiliwa na pingamizi, ninaweza kusimama katika Jina la Bwana, na kusema, “Hapa, Shetani, afadhali uondoke njiani kwa sababu haya ni mapenzi ya Bwana, mnaona. Naja katika Jina la Bwana Yesu, na—nawe inakubidi kuondoka njiani.”

²⁶ Na kama tukiangalia tu huduma yetu namna hiyo, na kufanya tu yale Mungu anayokwambia ufanye, haidhuru kama inaonekana sawa au si sawa iwapo Mungu anakuongoza, endelea tu kusonga mbele, unaona. Itaninii... Jambo la kwanza la kuwazia, “Je, ni mapenzi ya Mungu?” Halafu nia na kusudi lako. Kama kusudi lako ni sahihi na nia yako ni sahihi, halafu uambie mlima huu, “Ng’oka,” nao utang’oka. Hiyo ni kweli. Yakiwa ni mapenzi ya Mungu, na kusudi lako ni sawa, na nia yako ni sawa, itabidi ung’oke.

²⁷ Mmekuwa na subira, nasi tunawashukuru sana. Na sasa, pia tunataka kuwashukuru wadhamini wa wakfu huu, ama vyovyote unavyoongozwa hapa, kwa kuturuhusu kuja kwenye uwanja huu wa maonyesho hapa, kufanyia mkutano wetu hapa, ninathamini hilo. Ninathamini huyu mlinzi mzuri, ama—ama bawabu hapa nje, jamaa mwenye urafiki mwingi, sikuzote anapunga mkono na ni mzuri sana.

²⁸ Na—na kila kitu, muziki, nilimsikia Dada Fife, Olivia Fife, akiimba, kutoka, kuja kutoka Los Angeles, hapa juu. Hilo

ni zuri sana, Dada, hakika ninathamini hilo. Na marafiki zangu wote kutoka sehemu mbalimbali za nchi, Fresno, Bakersfield, na wa huku ambao wamekuwa wakitutembelea, hakika tunawashukuru kwa mioyo yetu yote.

²⁹ Na kama nimeacha chochote, mbona, mnisamehe, na—nawatakeni mjue ya kwamba kweli tunathamini kila kitu ambacho kimefanywa, kila jitihada. Na tunawaomba tu mtuombee sasa, tunapoendelea.

³⁰ Na sasa, ninaona lesa kadhaa zimewekwa hapa zipate kuombewa. Mbona, hakika tunafanya hivyo. Na kama hukuleta lesa yako hapa, niandikie tu: Jeffersonville, Indiana, Sanduku la Posta 325. Na sasa, utaipata, utarudishiwa le—lesa. (Asante.) Tunapata... Utapata, si lesa, maana siwezi kumudu kuzituma, zina—zinagharimu yapata senti kumi na tano, ishirini kila moja, na maelfu ya hizo kwa mwezi, unajua unakoenda, siwezi kuimudu. Lakini nina utepe, na vitu vidogo ambavyo dada fulani hunitengenezea, na kuuchukua, anavikatakata, na kuvitengeneza.

³¹ Sasa, utapata barua ya kawaida tu kutoka kwa katibu. Naye ataishughulikia, kwa sababu ni maombi ya ulimwengu mzima yanayoendelea wakati wote, inakwambia la kufanya, jinsi ya kutumia kitambaa hiki cha maombi. Na kama unataka kimoja, nawe huna haja nacho sasa, agizia, chukua kimoja, kiweke katika Biblia yako kwenye—kwenye Matendo mlango wa 19, itakwambia la kufanya nacho. Ndipo basi ukiweke humo, mtoto mchanga akiamka akiwa mgonjwa usiku, mtu fulani akiumia, chukua kitambaa hicho uwawekee, uone kitakachotukia. Amini tu. Unaona? Na hiyo itakuwa ndiyo ishara yako.

³² Hakuna malipo, hakuna kulipia chochote, agiza tu na ukipokee. Hivyo tu. Tuandikie tu kwenye, kama huwezi kuikumbuka hiyo namba, 325, basi wazia tu dola tatu na senti ishirini na tano. Na kama huwezi kuwazia hizo, andika tu Jeffersonville, Indiana, kila mtu ananijua, hata kwa polisi, na kwa hiyo watahakikisha kwamba ninakupata. Kwa hiyo, wewe kitume tu, nasi tutafurahia kukuhudumia. Naam, wanakuja kanisani mwangu, wengi wao, hakimu huja kanisani mwangu, na tu—tunafanya ushirika na watu wote walio karibu.

³³ Ndipo likiwapo lolote kuhusu hayo maono, ama chochote kile, kama lolote la mambo hayo linaleta swali, mnashangaa ni wapi tu...kwa nini msije, Jeffersonville na kuwauliza baadhi ya maofisa karibu na jiji hilo? Mwone kama maono haya yamekuwako daima, mwone kama kamwe yanashindwa, ama mtu fulani aingie mikutanoni, na kuangalia, aone kama yanashindwa kamwe, bila shaka hayashindwi.

³⁴ Wameketi kwenye mikahawa, wakiendesha barabarani, popote pale, mnaona tu u—u—upande wake ulio mdogo hapa, mnaona, mistarini, kwa sababu hiyo ni wewe unayefanya hivyo

hata hivyo, unaona, imani yako ndiyo inayosababisha hayo. Mungu anapoitumia, kwa kawaida ni jambo kuu ambapo Yeye hujua mwisho tangu mwanzo.

³⁵ Nilikuwa nimeketi chumbani muda mfupi uliopita nikizungumza na Ndugu yangu mpendwa Arganbright, *pale*, tu—tulikuwa tukizungumza kuhusu jinsi hilo hutukia, jinsi lilivyotukia, jinsi hilo linavyoweza kusimuliwa kabla hata halijatimia. “Ni kwa njia gani wewe...?” Akasema, “Kamwe si—sielewi, kuona jinsi unavyoweza kuketi hapa na kusema mambo yatakayotukia kesho.” Mnaona? “Jinsi itakavyotukia juma lijalo, ambapo utamwona mtu, kile atakachokuwa akifanya, kile kitakachotukia wakati... Na maswali yale yale atakayokuuliza, na hali hasa utakayomkuta *huyu* na...” Vema, ni Roho Mtakatifu, Yeye—Yeye aliahidi. Sasa, Yeye hatuambii mambo yote, Yeye hutuambia tu chochote anachotaka tujue.

³⁶ Sasa, kama ungesema, “Ndugu Branham, Yeye atasema nini kunihusu mimi?” Sijui. “Atasema nini...? Je, Yeye hukwambia kila kitu, na kukuacha ukwepe matatizo?” La, bwana. Mara nyingi ninaingia moja kwa moja ndani yake, kichwa juu ya visigino. Hiyo ni kweli.

³⁷ Vipi kuhusu...? Vipi kama mama yangu alikuwa amelala hapa akifa, na kusema, “Mwanangu, niliondoka mezani nikiwa na njaa mara nyingi, ili mpate chakula, nilikunyonyesha kwa titi langu wakati ulipokuwa mtoto mchanga. Nitapata afya au la?” Nisingejua, nisingeweza kusema, ingenibidi tu kumwomba Baba yetu wa Mbinguni. Kama Yeye aliniambia, ningeweza kumwambia mama yangu, kama hakuniambia, nisingeweza kumwambia, maana sijui. Mnaona? Ninaninii tu...

³⁸ Yote ni mamlaka, yako ndani Yake, mwanadamu hana uhusiano wowote nayo, kwa hiyo basi nina furaha sana kwamba Mungu aliifanya namna hiyo. Kwa hiyo sisi sote, hilo linatuweka sisi kila mmoja... Yeye angeweza kuzungumza nawe na kusema jambo lile lile, unaona, haijalishi. Kwa hiyo hakuna mmoja wetu aliye mkubwa ama mkuu, sisi sote ni watoto wadogo tu wa Mungu, mnaona, sisi kila mmoja ni watoto wa Mungu. Naye anatushughulikia kwa njia tofauti, lakini ni Baba yeye yule wa Mbinguni anayeshughulika.

³⁹ Sasa, leo, tulisema tungeombea kadi hizo zote za maombi tulizosambaza. Ndipo nikamwambia Billy, “Ni ngapi zilizotolewa?”

⁴⁰ Akasema, “Loo, yapata mia nne ama mia tano, hivyo tu.” Kwa hiyo, ndipo akasema muda mfupi uliopita, kasema, “Unajua nilisambaza nyingi sana,” kasema, “Ilinibidi kuwaleta wavulana waje kunisaidia kumpa kila mtu kadi ya maombi.” Kwa hiyo afadhali nianze, sivyo? La sivyo hatutamaliza. Lakini sisi... Bwana atatusaidia. Nimengeojea siku zote tano kwa ajili

ya saa ii hii sasa, kufikia ambapo jambo fulani litatendeka kama tu tutaliacha litendeke.

⁴¹ Sasa, tunajua ya kwamba karama na miito havina majuto, nasi tunaweza tu kufanya kadiri tutakavyomruhusu Mungu kufanya. Na sasa, sisi sote tunajua ya kwamba uponyaji wa Kiungu si kitu ambacho m—mhubiri hubeba kwenye mkoba, ama si kitu fulani alichu nacho mikononi mwake, uponyaji wa Kiungu ni imani yako mwenyewe katika kazi iliyomalizika ambayo Kristo alikufanyia pale Kalvari. Unaona? Ni jambo ambalo Mungu alikufanyia.

⁴² Nafikiri Ndugu Borders alisoma Maandiko muda mfupi uliopita, Waebrania, ama, Warumi mlango wa 4, kuhusu Ibrahimu. Nami nataka kuchukua somo alasiri ya leo linalopatikana katika Mwanzo 22, mlango wa 22 wa Mwanzo na kifungu cha 14, nasi tutasoma.

⁴³ Lakini kabla tu hatujasoma, tunapaswa kumwendea Kristo, kwanza, kwa maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu. Ni wangapi wanataka kukumbuka? Inueni mikono yenu, na kusema, “Mungu, unirehemu.”

⁴⁴ Baba yetu wa Mbinguni, tunapokuja kwa unyenyekevu sana katika Jina la Bwana Yesu, nikiutazama umati huu mzuri sana, na kushangaa tu kama tutawahi kukutana tena. Ninawaangalia, nawazia, “Sijui kama nitawahi kuwaona wote tena, namna hii?” Huenda nisiwaone. Kama nikirudi tena katika mwaka mmoja tangu sasa, hapana shaka ila wengi hapa hawatakuwa hapa wakati huo. Nami ninatambua basi kwamba mambo nisemayo yataninii, nitayajibia kwenye Siku ya Hukumu. Huenda nisiwe hapa, mimi mwenyewe, mwaka mmoja tangu leo, labda hakuna mmoja wetu atakayekuwa, Yesu anaweza kuja wakati wowote. Na atakapokuja, tutaenda nyumbani pamoja Naye, kwa sababu Yeye alituahidi tungeweza kwenda.

⁴⁵ Lakini kuna wengine hapa ndani, labda, Bwana, wasiokujua Wewe, wala hawako tayari kwenda, hao ndio tunaotaka kushughulikia, sasa hivi. Ninaomba ya kwamba jambo fulani litatukia alasiri ya leo, litakaloigeuza mioyo yao Kwako.

⁴⁶ Ninawaomba wote walioinua mikono yao, wengi wa hao walikuwa ni Wakristo waliojazwa na Roho, bila shaka idadi kubwa zaidi walikuwa, nao ni wagonjwa na wahitaji. Ee Yehova Mungu Mkuu, watimizie kila haja yao, na hiyo itakuwa ni imani ya kuamini kazi iliyomalizika imetimizwa.

⁴⁷ Sasa, kwa ibada hizi nne zilizopita tumejaribu sana, Bwana, kuweka imani ya watu hawa kwenye kazi iliyomalizika iliyofanywa pale Kalvari, na ahadi ambayo Mungu alitoa, na ambayo Kristo alifanya, na mitume walifanya, na manabii walitoa kuhusu siku hizi. Nasi tunakushukuru sana, Bwana, ya kwamba umethibitisha kila neno lake kuwa ni kweli. Sasa,

tunajua ya kwamba Wewe upo hapa; hawa watu wanangojea kuombewa.

⁴⁸ Sasa, tunapochukua somo hili, tunaomba ya kwamba—ya kwamba utalifanya lizae, jalia litimize yale liliyokusudiwa. Tubariki pamoja, Baba, tunapokungojea Wewe sasa, kwa ajili ya huduma ya Neno. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁹ Na sasa katika Mwanzo 22:14:

Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo... , Katika mlima wa BWANA itapatikana.

⁵⁰ Sasa nataka kuchukua Jina moja la Yehova: *Yehova-Yire*. Mungu ana Majina saba ambatani, ya ukombozi: *Yehova-Yire*, “Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu”; *Yehova-Rafa*, “Bwana akuponyaye”; na *Yehova-Manase*, na kadhalika, “Ngao yetu, Bendera yetu.”

⁵¹ Nayo Majina hayo hayatenganishwi, kama Yeye ni Yehova-Yire, basi Yeye ni Yehova-Rafa pia. Mnaona? Na kwa hiyo, huwezi kuyatenganisha Majina hayo ya ukombozi. Na kama Yehova-Rafa halikutumiwa kwa Yesu, wala Yehova-Yire halikutumiwa, Kwake, kwa hiyo kama Yeye si Mponyaji, Yeye si Mwokozi. Kwa hiyo, na kama Yeye ni Mwokozi, Yeye pia ni Mponyaji, na ni kazi iliyomalizika.

⁵² Sasa, tunazungumza juu ya Ibrahimu na Yehova-yire. Nalo neno *yire* linamaanisha, “Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu.”

⁵³ Sasa, tunaona katika kuzungumza juu ya Ibrahimu... Ninayo Maandiko machache mbalimbali kutoka Mwanzo 12, 15, 17, 18, na 20, na 22, ninataka tu kugusia sehemu muhimu za Maandiko hayo, mambo muhimu, na kuyaunganisha pamoja kwa ajili ya kutoka kidogo alasiri ya leo juu ya fundisho letu, ili tuweze kuliweka wazi kabisa, ili kwamba kweli mweze kuwa na imani.

⁵⁴ Sasa, nataka kila mtu, hasa ninyi mtakaoombewa, ama wewe unayemwomba mtu mwingine, kusikiliza kwa makini sasa, maisha ya Ibrahimu.

⁵⁵ Sasa, agano lilifanywa pamoja na Ibrahimu, na si kwa Ibrahimu tu, bali Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Ndipo basi hatuna budi kukumbuka ya kwamba sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Myahudi si *Myahudi*, ambaye kwa utaifa ni Myahudi, Myahudi ni *Myahudi* kwa ndani, Yeye ni Uzao wa Ibrahimu wakati anapomchukua Kristo, anakuwa Uzao wa Ibrahimu, naye yuko katika agano pamoja na Ibrahimu, kwa kuwa ahadi ilifanywa kwa Ibrahimu.

⁵⁶ Sasa, tunakuwaje Uzao wa Ibrahimu? Tunapokuwa na imani aliyokuwa nayo Ibrahimu. Ukiangalia, wakati Ndugu Borders akiyasoma Maandiko, hivi jambo hili lilimjia Ibrahimu alipokuwa katika tohara, au nje ya tohara? Alipokuwa... Kabla

hajatahiriwa. Kwa hiyo mnaona, matendo hayatupeleki popote, imani yetu ndiyo inayotuokoa.

⁵⁷ Nami na—nawatakeni mwone ya kwamba Ibrahimu alimwamini Mungu, ndipo ikahesabiwa kwake, ama, ikahesabiwa kuwa haki, kwa sababu alimwamini Mungu. Sasa, yeye alifanya nini? Tukichukua somo la Maandiko, “Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu.”

⁵⁸ Sasa, kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu, sasa, sikilizeni kwa makini sasa, itaumiza, kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu hakuna kitu kitakachotuyumbishia mbali na ahadi ya Mungu. Haidhuru ni kitu gani kinachotokea, ama ni nani anayesema vinginevyo, Uzao wa Ibrahimu kamwe hautaondoka kwenye ahadi hiyo, iwapo wewe ni Uzao wa Ibrahimu. Lakini kama ukisitasita, na kuondoka, na kusema, “Vema, sikulipata, mimi . . . hapana shaka ni kwa ajili ya kizazi kingine, kamwe hainifanyii kazi.” Huo si Uzao wa Ibrahimu, basi ujuzi wako una kasoro.

⁵⁹ Mungu anapotoa ahadi, Mungu hana budi kutimiza ahadi hiyo, asipoitimiza ahadi hiyo, basi Yeye si Mungu. Lakini kama akitimiza ahadi hiyo, njia pekee inayoweza kuishi ni kwa imani yako kuifanya iishi. Neno la Mungu ni Mbegu.

⁶⁰ Na kama vile Mungu alivyompa Ibrahimu ahadi, nasi tumekuwa na maelfu ya miaka ya ujuzi tangu Ibrahimu, lakini Ibrahimu alifanya ahadi kwa, ama, Mungu aliifanya kwa Ibrahimu na kwa Uzao wake baada yake. Mnaelewa? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kwa Ibrahimu, *na*, kiunganishi huunganisha hiyo sentensi pamoja, Ibrahimu *na* Uzao wake baada yake. Si *wazao* wake, bali *Uzao* wake, Uzao wa Yule ambaye Ibrahimu aliamini kwamba yuaja kwa imani. Kupitia huyo akaja Isaka, kupitia Isaka akaja Kristo, kupitia Kristo tukaja mimi na wewe.

⁶¹ *Uzao* wa Ibrahimu, si *wazao* kama *wengi*, bali *Uzao*, Uzao wa ahadi. Ibrahimu alikuwa na wana kadhaa, Ishmaeli, kisha akawa na wana saba kwa mwanamke mwingine, baada ya Sara kufa, mbali na binti. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba ilifanyiwa Uzao wa Ibrahimu, yule Uzao ambaye yeye aliamini kwamba angekuja kwa mwanamke huru, ambaye alikuwa tasa wakati huo.

⁶² Sasa, hebu tuliwekee msingi kidogo tu. Sasa, ninii . . . Tutaanzia kwenye Mwanzo 12, na kuendeleza hadi kwenye huu Mwanzo 22:14. Sasa, angalieni ya kwamba . . . Ni wangapi sasa wanaoweza kuelewa ya kwamba sisi tukiwa tumekufa katika Kristo ni Wazao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja naye sawasawa na ile ahadi? Inueni mikono yenu. Vema.

⁶³ Sisi tukiwa tumekufa katika Kristo, huko ni kufa kwa mambo ya ulimwengu, basi tunapaswa kuwa na tabia ya namna gani? Sijui, tunapaswa kuwa nini, tunapaswa kuwa mtu wa

namna gani kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu, na tu warithi pamoja na Kristo, pamoja naye katika ahadi? Tabia zetu na jinsi tunavyotenda huonyesha kile tulicho nacho ndani yetu.

⁶⁴ Tukisema tunamwamini Mungu na kisha tusite katika ile ahadi, na kusema, “Vema, sikuipata.” Basi sisi si Uzao wa Ibrahimu. Kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu, halafu tuondoke na kufanya mambo ya ulimwengu, tunakiri tu kuwa Uzao wa Ibrahimu, na *sio* Uzao wa Ibrahimu. Mnaona? Ibrahimu hakisita katika ahadi ya Mungu.

⁶⁵ Miaka mingi iliyopita, nikizungumza juu ya tabia... Kwa kawaida wanafuata ilia kuhusu jinsi ninavyoikemea ta—tabia ya kanisa, inapaswa kufanyiwa mapinduzi na kuinuliwa tena. Kwa sababu ninajua wakati kanisa linapoanza kupoteza sifa zake, tabia yake imeondoka pamoja na sifa yake, linadidimia. Wakati tabia yake inapoondoka, sifa zake huambatana nayo, kwa sababu wanapoanza kutenda kama ulimwengu, na kuonekana kama ulimwengu, na kushirikiana na ulimwengu, Kristo hutoka, ndipo ulimwengu unaingia.

⁶⁶ Mimi ni wa kusini. Nami... Huko chini katika majimbo ya kusini, miaka mingi iliyopita, walikuwa wakileta watumwa kutoka Afrika, Makaburu waliwaleta, kisha wakawauza huko kusini kwa, kama farasi wa kazi.

⁶⁷ Nami hakika ninaamini ya kwamba Abraham Lincoln alikuwa mmoja wa Marais wakuu sana tuliopata kuwa nao kwa kumweka huru mtumwa. Mungu kamwe hakukusudia mtu yeyote kuwa mtumwa. Si rangi yake, wala kanuni yake ya imani, yeye, haidhuru nini, kamwe hapaswi kuwa mtumwa. Mungu alimwumba mwanadamu kwa mfano Wake Mwenyewe, katika sura Yake. Mwanadamu alifanya watumwa, sio Mungu.

⁶⁸ Basi walikuwa wakiwaleta watumwa huku na kuwauza, nawe ungeweza kuwanunua kama vile unavyonunua gari la mtumba kwenye uwanja wa magari. Madalali wangepitia na kuwanunua, kisha waingie kwenye mashamba makubwa na kuwabadilisha. Kumchukua mwanamume mkubwa mno, mnene, na labda mke wake ni maskini mwanamke mwembamba sana, mbona, wanamnunua tu mwanamke mkubwa zaidi, na kumzalisha mwanamume huyu mkubwa kwa mwanamke huyu mkubwa wapate kufanya watumwa wakubwa zaidi, kama ng’ombe. Unamaanisha hilo lingempendeza Mungu? La, bwana. Hakuna mtu anayeweza kuwa Mkristo na kuamini katika utumwa.

⁶⁹ Wakati fulani uliopita katika jumba fulani la makumbusho nilikuwa nikitembea siku moja, nikamwona mzee mweusi mwenye mzingo mdogo tu wa nywele kichwani mwake, nyeupe kama sufu juu ya kondoo, naye alikuwa akiangalia, alikuwa ameshika kofia yake mkononi mwake, ndipo baada ya kitambo kidogo akaangalia juu ya kitu kidogo cha kioo, naye akaruka nyuma upesi sana, machozi yakaanza kutiririka mashavuni

mwake, naye akafanya, ilionekana kana kwamba alikuwa akiomba.

Nilimwangalia huyo mzee kwa dakika chache, nikamwendea, nikasema, “Mjomba,” nikasema, “u—una—unaombea nini? Kwa nini ukasisimkwa?”

Akaniangalia kigeni sana, akasema, “Nilikuwa nikimshukuru Mungu.”

Nikasema, “Kumshukuru Mungu kwa nini, naomba niulize?” Nikasema, “Mimi ni mhudumu, ningetaka kujua, ninii tu, nilikuangalia tu.”

Akasema, “Njoo hapa.” Kasema, “Angalia *pale*.”

Nikasema, “Sioni chochote ila nguo, nguo ya mwanamke.”

Akasema, “Lakini unaona lile doa hapo juu?”

“Naam.”

⁷⁰ Akasema, “Hiyo ni damu ya Abraham Lincoln.” Akasema, “Kama ungeweza kuweka mikono yako ubavuni mwangu, ungehisi alama za mshipi wa utumwa.” Akasema, “Damu hiyo iliniondolea mshipi wa utumwa.”

⁷¹ Nikawazia, “Kama mnegro angeweza kujisikia hivyo kuhusu damu ya Abraham Lincoln iliyomwondolea mshipi wa utumwa, Mkristo anapaswa kufanya nini anapoiona Damu ya Yesu Kristo, aliyeitoa nafsi yake kutoka kuzimu, nafsi yake kutoka utumwani, mambo ya ulimwengu? Kwa nini turudi na kuwa watumwa wa ibilisi tena?”

⁷² Walikuwa wakiwanunua hawa watu weusi kwa, wakapata hati yao kama tu vile ungepata, ama bili ya mauzo. Siku moja dalali mmoja akapitia kwenye shamba fulani, akasema, katika shamba hili, akasema, “Una watumwa wowote wa kuuza?”

Kasema, “Vema, nina kama mia moja hapa nje, kwa hiyo unaweza kuwachunguza, labda tufanye biashara.”

⁷³ Nao, hao watu walipotoka kwenye nchi ya uenyeji wao, wakaja huku kutoka Afrika, wali—walisikitika, na walikuwa na huzuni. Wao wangewacharaza kuwafanya wafanye kazi, wangechukua mjeledi mkubwa, na kuwapiga wapate kuwalazimisha wafanye kazi. Hawakutaka kufanya kazi, maana hawakuwa na ujasiri wa kufanya kazi, walikuwa tu wameishiwa na ujasiri.

⁷⁴ Nao waliona, wakati dalali huyu alipokuwa akitembea—tembea, kulikuwa na jamaa mmoja mwenye sura nzuri, mkubwa, jamaa mwenye nguvu, kijana, haikuwalazimu kumcharaza, alikuwa ameweka kifua mbele, kidevu chake juu, alikuwa chonjo na ni mchapa kazi.

Kwa hiyo dalali akasema, “Aisee, ningetaka kumnunua mtumwa yule.”

Lakini mwenye mali akasema, “Hauzwi.”

Akasema, “Je, yeye ndiye boshi wa hao wengine wote?”

Akasema, “La, yeye ni mtumwa.”

Kasema, “Yeye ni...?” Kasema, “Labda unamlisha tofauti kidogo na hao wengine?”

Kasema, “La, wote wanakulia huko nje manchani pamoja.”

Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao watumwa wengine?”

⁷⁵ Akasema, “Mara nyingi nilishangaa, pia, mpaka nilipopata habari zake.” Akasema, “Unaona, huko katika nchi ya uenyeyi baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila, na ingawa yeye ni mgeni, hata hivyo anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye anatenda kama mmoja.”

⁷⁶ Kama mnero aliyekuwa utumwani angeweza kujua ya kwamba baba yake alikuwa mfalme wa kabila, ni mwenendo wa namna gani mwanamume ama mwanamke, anayejua ya kwamba Mungu ndiye Mfalme wetu, ingawa sisi ni wageni tukitembea hapa katika nchi hii? Wasafiri na wageni tukikiri sisi ni Uzao wa Ibrahimu, tunaotazamia Mji ambao mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu, ambao utakuja siku moja.

⁷⁷ Mwenendo wetu wote unapaswa kuwaje? Sio kama ulimwengu, bali tunapaswa kutenda kama wana na binti za Mungu, tuenende kama watoto wa Mfalme, sio kama watumwa wa mitindo, na watumwa wa tamaa, na watumwa wa kiburi. Nasi tunapaswa kuwa wana na binti za Mungu, na kutenda kama wao, na kujiendeleza hivyo, mazungumzo yetu, na kila kitu, na yakolee kwa Roho wa Mungu.

⁷⁸ Agano lilitolewa kwa Ibrahimu na kwa Uzao wake, sasa angalieni, lile agano lilikuwa ni neema tupu, kabisa. Hakukuwa na, “kama utafanya,” ama, “kama hutafanya,” ama, “ukifanya hivi, nitafanya hivi,” alisema, “Tayari nimefanya hivyo,” si, “kama utafanya jambo fulani.”

⁷⁹ Alifanya agano na Adamu naye akalivunja. Kila wakati mwanadamu anapofanya agano na Mungu, mwanadamu huvunja agano lake, lakini Mungu alikusudia kumwokoa mwanadamu, kwa hiyo akafanya agano hili bila masharti na Ibrahimu, loo, hili hapa, Ibrahimu na Uzao wake, mnaona, hilo agano limetolewa kwako bila masharti, si, “ukifanya,” “nimefanya.”

⁸⁰ Kwa hiyo si lazima useme, “Kama—kama—kama—kama—kama, Bwana, kama—kama nikifanya hili ama kufanya lile Wewe utaniponya?” Tayari amelifanya, halina masharti, tayari amelifanya, inakubidi tu kulikubali.

⁸¹ Roho wa Mungu ndani yako anaita, unasema, “Mungu, hivi Wewe...?” Ni kama tu maskini mama huyu kwenye kitanda cha wagonjwa hapa, mvulana huyu mdogo, mwenye sura nzuri aliyeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, mama

akitetemeka kwa kupooza, “Mungu nifanye nini kukufanya uniponye?” Tayari amekuponya, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kufanyika tu Uzao wa Ibrahimu. Unafanyaaje hilo? Kwa kumwamini Bwana Yesu Kristo na kujazwa na Roho, ndivyo ilivyo, halina masharti.

⁸² “Itanibidi kufanya nini kufanya hivyo?” Si chochote ila kuamini, hivyo tu. Likubali tu, liko papo hapo mbele zako, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kunyosha mkono na kulichukua, useme, “Ni langu, Mungu alinipa mimi,” halafu usisitesite nalo, hata iweje.

⁸³ Baada ya kuombewa, usitoke nje na kusema, “Vema, kamwe sikuhisi chochote.” Sasa, wakati wewe, kama ukiweka hilo—hilo ndani yako, hata kama kitu chochote kinakwambia hivyo, unajua ni ibilisi, kwa sababu umeponywa, umeponywa bila masharti.

⁸⁴ Unasema, “Vema, sistahili kuponywa.” La, wala mimi pia, hakuna mwingine anayestahili. Lakini si kile ulicho, ni kile Yeye alichu. Loo, jamani! Usijiangalie mwenyewe, angalia ile Dhabihu.

⁸⁵ Vipi kama, huko nyuma katika Agano la Kale, ama chini ya sheria za dhabihu, vipi kama nyumbu mdogo angezaliwa, na maskini nyumbu huyo angekuwa na masikio yaliyoinama, macho yake yana makengeza, magoti yake yamepindika, mkia wake umesimama moja kwa moja juu? Vema, ni kiumbe cha kuchukiza jinsi gani!

⁸⁶ Kama maskini jamaa huyo angeweza kuangalia kote, angesema, “Vema, kamwe hawatanilisha, sistahili kulishwa, la, bwana, kwa sababu hebu angalieni masikio haya.” Sasa, nyumbu yeyote mwenye masikio yaliyoinama ni nyumbu mbaya. Ati macho yenye makengeza? Magoti yaliyopinda? Hafai hata kidogo.

⁸⁷ Angesema, “Vema, na—nadhani mara tu bwana anayenimiliki atakapotokea, mbona, atachukua tu shoka na kunipiga kichwani, maana sistahili kulishwa.” La, hastahili.

Lakini vipi kama maskini huyo mama yake angeweza kuzungunza? Aseme, “Hebu kidogo, Mpenzi, ninataka kukwambia jambo fulani, unaona. Utaishi.”

“Kwa nini, Mama?”

⁸⁸ “Kwa sababu wewe ndiwe kifungua mimba changu, una haki ya mzaliwa wa kwanza. M—mwenyewe ataninii, kuhani kamwe hatakuangalia aone kama wewe ni mzuri au la, lakini ili uweze kuishi, itabidi kuwe na mwana-kondoo ambaye hana budi kuwa asiye na ila, kuchukua mahali pako.”

⁸⁹ Usijiangalie mwenyewe, mwangalie Mwana-kondoo wako. Mungu hakukubali wewe, Yeye alimkubali Mwana-kondoo, naye Mwana-kondoo alipachukua mahali pako. Ee Mungu! Hivi

hamwezi kuliona? Si wewe, wewe hustahili, mimi sistahili, hakuna mmoja wetu anayestahili. Lakini, mnaona, Yeye anastahili? Mungu alisema hivyo, alimkubali, akasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa Naye; huyu ni Mwanangu, msikieni Yeye,” kwenye siku ya kufanywa wana wenye mamlaka, “huyu Ndiye.”

⁹⁰ Usiseme, “Vema, daktari anasema kamwe sitapona.” Hivyo ndivyo daktari asemavyo. Sasa, mtu huyu ni mtu wa kisayansi, anaangalia jinsi maumbile yanavyoendelea, naye anaona huwezi kamwe kupona, hiyo inamwonyesha hilo kisayansi. Vema, hilo ndilo analoangalia, kama ukiangalia jambo lile lile, kamwe hutapona. Lakini usiangalie kile alichosema, usiangalie kile wewe. . . jinsi unavyopungua, bali angalia Sadaka yako. Jambo ndilo hilo.

⁹¹ Pia kumbuka wewe ni Uzao wa Ibrahimu na mrithi pamoja naye, basi kama ndivyo ulivyo, dumu na hiyo ahadi, mkubali Yeye kama Mponyaji wako, na ukae tu papo hapo. Ibrahimu aliliamini, nayo ilimchukua miaka ishirini na mitano kabla mtoto huyo hajazaliwa, lakini badala ya kuwa mnyonge, kila siku alipata nguvu, nguvu zaidi. Naam, bwana.

⁹² Ninaweza tu kuwazia, sasa, hili, natumaini halionekani la kukufuru, lakini waweza kuwazia mzee sasa? Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano wakati Mungu alipomjia, alipokutana naye, mke wake, Sara, alikuwa na sitini na mitano, hawakuwa na watoto, mke alikuwa tasa, yeye alikuwa mgumba, kwa hiyo hawakuwa na watoto. Ndipo Mungu akasema, “Ibrahimu, nitakupa mtoto kwa mkeo, Sara, Na kupitia kwa Uzao huo nitayaokoa mataifa yote. Hiyo itaninii. . . Utakuwa ninii—utakuwa baba wa mataifa mengi.”

⁹³ Sasa, ungeweza kuwazia mzee akishuka kwenda kwa daktari pamoja na mkewe wa miaka sitini na mitano, na kuweka nafasi hospitalini akamzae mtoto?

⁹⁴ Unajua, unapomchukua Mungu. . . Kama wewe kweli ni Uzao wa Ibrahimu, mambo ya ulimwengu ni upumbavu kwako, nao walimwengu, wanafikiri wewe ni mpumbavu, kwa sababu ni—ni dunia mbili mbalimbali.

⁹⁵ Hapa hivi majuzi, vema, kiangazi kilichopita mimi na mke wangu tulikwenda dukani kununua cha—chakula, niliingia kutoka kwenye moja ya miamsho yangu, na—nami nikaona jambo la ajabu nchini mwangu, tulikuwa tukienda kwenye duka la vyakula, nami nikamwona mama mmoja aliyekuwa amevaa sketi, nikasema, “Jamani, yeye ni wa mtindo wa kale, sivyo?” Wengine wote walikuwa uchi tisa kwa kumi. Nikasema. . . Nami. . .

⁹⁶ Akasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani, Billy,” mke wangu akasema, akasema, “angalia, huyo—huyo—huyo mwanamke, watu hawa huimba katika kwaya, nao huenda

kanisani,” akasema, “ni kitu gani kinachowafanya wafanye hivyo?”

⁹⁷ Nikasema, “Wao si—wao si—wao si wa nchi hii.” Sasa, ukiingia Afrika, unapata roho ya Kiafrikana; ukienda Uswisi, unapata roho ya Uswisi; ukienda Ujerumani, unapata roho ya Kijerumani; ukija Marekani, unapata roho ya Kimarekani, hiyo ni mbali sana na kuwa Roho ya Mungu. Lakini basi ni nini kinachosababisha...?

⁹⁸ Unasema, “Wamarekani hawa wote hutenda hivyo?” Naam, hiyo ni roho ya Marekani. Lakini unapokuwa Uzao wa Ibrahimu, basi wewe si—wewe si tena... unaishi hapa, hili ni taifa lako, nawe unapaswa kushukuru kwa ajili yake, lakini kwa kweli wewe si Mmarekani, wewe ni Mkristo, na Roho yako inatoka Juu, kwa hiyo inakufanya utende kama wanavyofanya Huko juu, si kama wanavyofanya hapa chini, mtakatifu, safi, mwenye haki, mwenye upendo, kuheshimiana, upendo wa kiungu mmoja kwa mwingine, umezaliwa kutoka Juu, hiyo ndiyo sababu unatenda tofauti, kwa sababu Roho wako anatoka Huko juu.

⁹⁹ Sasa, Ibrahimu alipewa ahadi hii, na, labda, baada ya mwezi wa kwanza akamwambia Sara, “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

¹⁰⁰ “Mungu asifiwe, tutampata huyo mtoto mchanga, kwa vyovyote vile. Jitayarishe, nenda kanunue jicho ndege, na pini, na vijibuti, na kila kitu, tutampata.” Hakuna dalili yake, hata kidogo.

Akangojea siku zingine ishirini na nane, “Vipi kuhusu hilo, Sara?”

“Hakuna tofauti, Mpenzi.”

¹⁰¹ “Utukufu kwa Mungu, ungekuwa ni mwujiza mkubwa zaidi sasa, kama ungetukia mwezi uliopita.” Mnaona? Kujitayarisha kwa ajili yake. “Weka tu hizi pini, na kila kitu karibu, atakuja.”

Miaka kumi ikapita, “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu, ni miaka kumi zaidi, mwujiza mkubwa kuliko hapo awali! Tutampata, kwa vyovyote vile.” Akapata nguvu zaidi, badala ya kuwa dhaifu.

¹⁰² Baada ya miaka ishirini na mitano kupita, sasa yeye ana umri wa miaka mia moja naye mke ana tisini, “Vipi kuhusu hilo, Sara?”

“Hakuna tofauti.”

“Haleluya! Tutampata, kwa vyovyote vile.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.”

¹⁰³ Sasa, unaweza kuwazia hilo kuhusu uponyaji wako? Unaweza kuamini hilo kuhusu uponyaji wako, kijana mwanamume? Unaweza, Dada? Mnaweza huko nje? Haidhuru ni jambo gani linalotukia, Mungu alisema hivyo, hilo latosha, liamini. Hiyo ni imani halisi, hao ni watoto wa Ibrahimu. Kumbukeni, si kile ulicho, kile Yeye alich; angalia Dhabihu yako, daima.

¹⁰⁴ Sasa, katika Mwanzo 15, laiti tungalikuwa na muda mrefu zaidi, kudumu kwenye hilo, bali hatuna, Mwanzo 15, lile—lile agano lilithibitishwa kwake katika mlango wa 15. Sasa, kabla jambo hili halijafanywa, kabla lile agano halijathibitishwa, inakubidi kuingia katika utii kabisa.

¹⁰⁵ Sasa, Ibrahimu, Mungu alimwambia ajitenge na watu wake. Na, siku hizi, badala ya kujitenga na ulimwengu, tunajaribu kuuchukua ulimwengu pamoja nasi, Mungu anataka utengano. Kanisa, siku hizi, mnapompigia kura mchungaji wenu, kwa kweli m—mnataka, mnataka mchanganyaji. Loo, mnasema, “Mchungaji wetu ni mchanganyaji mzuri.” Vema, yeye si wa Mungu basi, Mungu anataka watenganishaji. Um-hum. Hiyo ni kweli, enyi watenganishaji.

¹⁰⁶ Mnasema, “Loo, yeye ni mchanganyaji mzuri, atacheza mchezo mdogo wa karata pamoja nasi, naye atafanya mizaha michache pamoja nasi, naye ata—atashuka ziwani na kuogelea pamoja nasi, na kuwachukua wasichana wote, na wazee, pia, na kulala hapo chini, wapate mbambuko wa jua, na—nanyi mwajua, yeye ni mchanganyaji mzuri.” Naam, naam, mnahitaji mbambuko wa mwana.

¹⁰⁷ Nina wasichana wawili, huenda wakafanya hivyo, pia, sijui, kama wakifanya hivyo, hakika watapata mbambuko. Sijui kama utatoka kwenye jua hilo *huko* juu, utatoka kwa Charles Branham, mwana wa baba yangu, mimi, kwa mkanda wa pipa kwa nguvu niwezavyo. Watapata mbambuko mzuri kweli, itawachukua muda mrefu, watakulia kwenye shubaka ya mekoni.

¹⁰⁸ Sasa angalieni, nawaambia, hatutaki—hatutaki wachanganyaji, tunataka watenganishaji, kujitenga, kujitenga na kutokuamini. Huyu mnayezurura naye, na kusema, “Loo, msilisikilize kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha, hakuna kitu kwake,” jitengeni nalo. Naam, bwana.

¹⁰⁹ Wewe ni mfuasi wa chama cha wanawake cha kushona na kushikiza, mwajua, ambapo wanashona na kushikiza, na kushona na kushikiza, na kushona na kushikiza, na kuzungumza juu ya Bibi *Nanii*, nao wanasema kule, wanasema, “Vema, sasa, nitawaambia, wakati mmoja ni—niliamini katika upuuzi huo wa watakatifu wanaojifingirisha, pia, lakini . . .” Jitenge na mambo hayo.

¹¹⁰ Chochote ambacho ni kinyume na Neno la Mungu, jitenge nacho, usijali ni kitu gani. “Ondokeni kati yao, msiguse kitu chao kilicho kichafu.” Hilo ni—hilo ni jambo zuri, la busara, tukinena kiroho, kufahamu. Biblia ilisema hivyo, “Ondokeni kati yao, msiguse vitu vyao vilivyo vichafu, nami nitawapokea.” Hawezi kuuleta ulimwengu, kamwe hatauleta. La, bwana. Unapotahiriwa, ulimwengu unakatiliwa mbali nawe, hiyo ni kweli, basi wewe ni Uzao wa Ibrahimu.

¹¹¹ Mungu ametambua ahadi Yake kama alivyofanya na Ibrahimu, akamtahiri. Na hivyo ndivyo ilivyo wakati Mungu anapoitambua imani yako, ndipo anaukatilia mbali ulimwengu kutoka kwako, na kukupa Roho Mtakatifu, nawe kweli unamwamini Mungu basi kwa lolote Yeye asemalo, hiyo ni kweli. Mpaka wakati huo, wewe ni mtangaza imani tu, si mmiliki.

¹¹² Sasa, angalieni kilichotukia, naye akasema, “Nitajuaje mambo haya?” Ibrahimu alijua.

Sasa ninawatakeni msikilize kwa makini sana, ndugu, kwa dakika moja.

¹¹³ Akasema, “Nitakwambia jinsi nitakavyofanya jambo hilo.” Sasa, hilo agano lilifanywa bila masharti, bali Yeye alisema, “Nitakuonyesha jinsi nitakavyokuthibitisha hilo, kukwambia jinsi nitakavyolifanya.”

¹¹⁴ Naye akaenda akamchukua ndama wa miaka mitatu na ko—kondoo wa miaka mitatu, na kadhalika, na kuwakatakata vipande, naye akachukua hua na njiwa, na ndipo akangojea mpaka giza lilipoingia, akawafukuza ndege wote kutoka kwao, Mungu aliahidi kukutana naye. Kwa hiyo, alipofanya hivyo, aliwafukuza ndege wote, giza likaanza kuingia, sasa angalieni kilichotukia, giza kuu likaja juu ya Ibrahimu, naye akashikwa na kitu kama usingizi.

¹¹⁵ Sasa, hilo ndilo lipasalo, sasa, kwa kila mwanadamu anayezaliwa. Sasa, angalieni kile Yeye, angalieni agano Lake sasa, jinsi alivyolithibitisha kwa Ibrahimu, hili linapaswa kuwafanya Wapresbiteri kupaza sauti. Sasa, yeye...Giza likaingia, halafu amezungukwa na giza, naye akaingia katika usingizi wa mauti, ingesemwa. Sasa, hapo ndipo kila mwanamume atafanya, atakufia, mwanamume, mwanamke, mvulana, ama mtoto, mauti iko mbele yako.

¹¹⁶ Lakini basi akaona mbele ya hapo kulikuwa na tanuru ya moshi, ambapo kila mwenye dhambi, na kila mwanamume, na kila mwanamke, mvulana au msichana anastahili kwenda, kuzimuni. Hiyo ni kusema, hiyo ilikuwa ni kule kuanguka kwetu, huko ndiko Adamu alikotushindilia, kwamba tunastahili kwenda jehanamu, kwa sababu tulizaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo, kwa hiyo hakuna mmoja wetu aliye mwenye haki, kwa hiyo hatuwezi kujitegemea wenyewe, tunaninii, tunamtegemea Yeye.

¹¹⁷ Mwenye hatia ya iliyo ndogo sana ana hatia ya yote, na Yeye anataka ukamilifu. Kwa hiyo unawezaje kukamilishwa? Huwezi kujiangalia na kukamilishwa, bali nilimwangelia Yule aliye mkamilifu, Yule aliyepachukua mahali pang'u, Yeye Ndiye mkamilifu.

¹¹⁸ Na sasa tunaona, ndipo upande wake wa pili ikatokea Nuru ndogo nyeupe, nao wakaingia moja kwa moja katikati ya dhabihu hizo. Sasa, kama tungalikuwa na wakati wa kuyafafanua yote, bali hatuna, ila ninawatakeni mwone kile alichokuwa anafanya pale.

¹¹⁹ Sasa, hiki *hapa* kipande kidogo cha karatasi, ninataka kukitumia hicho kwa muda kidogo. Sasa, sisi Wamarekani tunafanya nini tunapofanya a—agano, mmoja kwa mwingine? Kwa kawaida tunatoka, tunalizungumzia na kitu kama hiki: Tungesema, nami ningesema, kama kwa Ndugu Slater, “Ndugu Slater, nitafanya jambo *fulani-fulani*, kama utafanya jambo *fulani*.”

“Naam, naam.”

“Vema. Nitarudi juma lijalo.”

“Naam.”

“Vema. Hayo ni mapatano?”

“Naam.” Kisha tunapeana mikono. “Liweke *hapa*, jamani.” Hilo ni agano, tulifanya mapatano.

¹²⁰ Sasa, huko Japani wanapofanya agano wanasimama na kuongea wao kwa wao, na kama wakifanya ninii, wakiandika agano, na kufanya mapatano yao, mnajua wanafanya nini? Wanarushiana chumvi, mnaona, wanaarushiana chumvi. Chumvi ni ladha, mnaona, kama ikigusa. Kwa hiyo, wanaarushiana chumvi, hilo ni agano.

¹²¹ Lakini katika wakati wa Ibrahimu jinsi walivyofanya agano, walichukua karatasi ya ngozi, ama, kipande cha—cha—ngozi, nao wakaandika agano hili, wakaliandika, yale wangepanya, hayo ndiyo mapatano yao. Halafu wanamchinja mnyama, ambaye alikuwa ni dhabihu, wanamchinja mnyama, nao wanasimama katikati ya vipande hivi viwili. Na juu ya agano hili wanaapiana, kisha wanaipasua *hii*, mmoja anachukua kipande kimoja na mwingine kingine; huwezi kukinakili. Na wakati agano hilo, linapothibitishwa, ama, kuletwa pamoja tena, kila kipande cha karatasi hiyo hakina budi kuumana kikamilifu, mmoja akishikilia kipande kimoja, na mmoja akishikilia kingine.

¹²² Sasa, Mungu alikuwa akisema nini? Kwamba kupitia Uzao wa Ibrahimu, ambapo alikuja Isaka, kupitia Isaka akaja Yesu, na sasa, pale Kalvari, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa Imanueli, Mungu pamoja nasi, lakini pale Kalvari, Mungu alimpasua, alimpasua, kisha akaufufua huo mwili,

na kuuweka kwenye mkono Wake Mwenyewe wa kuume, na kumtuma Roho aliyekuwa katika huo mwili, arudi chini juu ya Kanisa kuendeleza kazi alizofanya mle ndani, hilo hapo agano lililothibitishwa.

¹²³ Kwa hiyo Kanisa litakalokuwa Bibi-arusi wa Yesu Kristo litabatizwa katika Roho yuyo huyo, pamoja na ishara ile ile, maajabu yale yale, Roho Mtakatifu yule yule aliyekuwa juu Yake atakuwa ndani ya Kanisa, haina budi kuwa sawa kabisa. Kwa hiyo wakati Roho huyo aliposhuka, alishuka kwenye Pentekoste, juu ya waaminio mia moja na ishirini, Naye akawabatiza katika Mwili wa Kristo. Ndipo Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu ya Kristo, akawa juu ya Kanisa, akaendelea, “Kitambo kidogo ulimwengu unaniona, tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, zaidi ya hizi mtazifanya, naenda kwa Baba Yangu.”

¹²⁴ Mnaona, Roho yeye yule akiuambia Uzao wa Ibrahimu, ya kwamba kupitia kwa uzao wa Ibrahimu alikuja Kristo, kwamba angemrarua, na kuweka Roho wa Mungu juu ya Kanisa Lake, na kuipeleka Dhabihu Nyumbani pamoja Naye. Amina! Ndugu, hilo linamfanya ibilisi aondoke, hilo litamweka mahali pake.

¹²⁵ Na kusema, “Loo, ninyi ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha, hamko *hivi*. M—mlifanya *hivi*.” Sijali kile umefanya, kwa neema, kwa ahadi ya Mungu, kwa Roho Mtakatifu, si kile ulicho, ni kile Dhabihu yako ilicho.

¹²⁶ “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Kwani unaogopa nini? Unaogopa nini?

Unasema, “Vema, labda mimi si Mkristo anayefaa.”

¹²⁷ Unawezaje kumjia Mungu bila Mungu kukuita kwanza? “Na wote aliotangulia kuwajua, amewaita.” Hiyo ni kweli? “Wote aliowaita, amewahesabia haki.” Hiyo ni kweli? “Wote aliowahesabia haki, amewaninii,” tayari, wakati uliopita, “amewatukuza.” Amina. Ni kazi iliyomalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Wakristo, hivi hamwoni mnaishi chini ya majaliwa yenu? Hamjui ninyi ni nani.

¹²⁸ Mara nyingi nimesema ninaona matabaka mawili ya watu: Moja ni la Kipentekoste, na moja la kimsingi. Aliye wa kimsingi anajua mahali anaposimama, bali hana imani; Mpentekoste anayo imani, wala hajui yeye ni nani.

¹²⁹ Ni kama tu mtu aliye na pesa kwenye benki, hawezi kuandika hundi; huyo mwingine anaweza kuandika hundi, wala hana pesa kwenye benki. Laiti mngaliweza kuwaleta pamoja! Kama ningeweza kuwafanya Wapentekoste kutambua ya kwamba wao ni wana na binti za Mungu, na warithi wa Ibrahimu, basi hakuna ibilisi, ama chochote kinachoweza kuwashikilia watu Wake. Mungu aliahidi hilo. Kama Yeye si

Mungu, liondokee, kama Yeye ni Mungu dumu nalo. Amina. Alilithibitisha hilo agano.

¹³⁰ Katika Mwanzo 17 Yeye alimtia nguvu Ibrahimu kwa ajili ya mwujiza. Hivyo ndivyo anavyofanya sasa, kuliimarisha Kanisa kwa ajili ya mwujiza. Alimtokea katika Mwanzo 17 katika Jina la *El Shaddai*. Inamaanisha, hapo inasema, “Mwenyezi Mungu,” neno la Kiebrania ni *El Shaddai*, “Mwenye nguvu,” ama *Shad* linamaanisha, “matiti,” kama titi la mwanamke. Lakini si tu *Shad*, *Shaddai*, maana yake, “mwenye matiti.”

¹³¹ Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, tisini na tisa, ndipo Mungu akamtokea, akasema, “Sasa, Ibrahimu, nilifanya hilo agano bila masharti, ulipojitenga, nilikubariki, nikakuonyesha yale nitakayofanya. Sasa una umri wa miaka mia moja, mke wako ana umri wa miaka tisini, sasa nitakwambia, hili hapa Jina Langu kwako: Mimi ni Mungu mwenye matiti.” Loo, jamani! Matiti mawili, Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.

¹³² Kama vile mtoto mchanga ambaye ni mgonjwa, a—a—a—afya yake imezorota, naye anahangaika na kulia, ndipo mama anamchukua huyo mtoto mchanga, na kumlaza kifuani mwake, anamshikilia hapo juu, ndipo huyo mtoto mchanga ananyonya nguvu za mama zinamwingia. Hivyo ndivyo ulivyo hapa, uliyeketi kitini, mama; hivyo ndivyo ulivyo, ewe kijana mwanamume, uliyeketi kwenye kiti cha magurudumu; hivyo ndivyo ulivyo huko nje ukiwa na kansa, wakati madaktari wanapokukatia tamaa; hivyo ndivyo ulivyo uliye na ugonjwa wa moyo, wowote ule, unaona, wewe ni Uzao wa Ibrahimu, Naye ni *El Shaddai*.

¹³³ Loo, kama una haja kwa ajili ya dhambi zako, tegemea ahadi hii, nyonya nguvu zako upate wokovu. Kama umerudi nyuma, rudi, uishikilie ile ahadi, na uinyoshe mpaka ujisikie umepata nguvu zaidi. Kama unahitaji uponyaji kwa ajili ya mwili wako, Yeye alikuwa... kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Nyonya titi hilo la *El Shaddai*, ahadi hiyo, mpaka nguvu zako zinapoanza kuongezeka, unaanza kujisikia wewe ni... .

¹³⁴ Na isitoshe, bali linaridhisha, titi la mwanamke humridhisha mtoto wake mchanga, nalo titi la Mungu lililoahidiwa linamridhisha mwaminio. Mradi tu Mungu alisema hivyo, inaleta tofauti gani? Ni mridhishaji, mpaji wa nguvu. Loo, jamani!

¹³⁵ Isitoshe, linamridhisha mtoto mchanga, hasumbui na kutatiza tena, hana nguvu kabisa, bali ameridhika mradi ana titi la mama yake (Loo, ndugu!), kunyonya nguvu zake, si nguvu zake, nguvu za mama. “Si mapenzi yangu, mapenzi Yako. Si yale ninayowazia, yale Wewe uliyosema.” Amina. Hilo hufanya hivyo. Kuridhisha, kuridhisha zaidi, kuegemea kifuani, kunyonya.

¹³⁶ Ibrahimu aliegemea moja kwa moja kwenye kifua hicho kwa muda wa miaka ishirini na mitano, kamwe hakukiachilia. Amina. Mama anawezaje kumtunza mtoto wake—Mama anawezaje kumdumisha mtoto wake ameridhika kama akiachilia ti—ti—titi lake wakati wote, akinyonya nguvu zake? Mtoto huyu anawezaje kupata afya na kupata nguvu, maadamu anajaribu, anajifanya anataka kunyonya, kisha anaondoka, hataninii. . . analikataa, tena? Jambo ndilo hilo.

¹³⁷ Loo, ndugu, hivi huoni huo ulikuwa ni—ni ujumbe wa jinsi gani kwa mtu mwenye umri wa miaka mia moja, akimwamini Mungu? Sasa—sasa, Biblia ilisema ninii ya—yake, alikuwa ni kama amekufa kama mwanaume, nalo tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa, kwa hiyo ni ahadi ya jinsi gani kusema, “Ibrahimu, nguvu zako kama mwanaume, zimekufa, na tumbo la uzazi la Sara limekufa, nanyi ni wakongwe, bali Mimi ndimi Mwenye nguvu, Mimi ndimi Titi. Wewe si zaidi ya mtoto mchanga, bali Mimi ndimi Mwenye matiti, ninatoa ahadi, ninaweza kukuimarisha tena.” Amina. Loo!

“Utafanya nini?”

“Waweke tayari kwa ajili ya mwujiza unaokaribia kutukia.”

¹³⁸ Sasa, ninataka kwenda kwenye Mwanzo mlango wa 18 na kuonyesha yale aliyofanya. “Mimi ndimi Mwenye matiti.” Mlango wa 18, mlango unaofuata, kumbukeni alikuwa ameketi nje mbele ya mlango wa hema yake, alikuwa na umri wa miaka mia moja wakati huo, Sara alikuwa na tisini.

¹³⁹ Sasa, wakati alipokuwa ameketi nje kwenye joto la mchana yapata saa tano, ama saa sita, mambo yalikuwa yakiharibika, angeshika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, labda hata hawakuwa na misheni, sembuse kanisa lenye kiyoyozi. Lakini walikuwa wameketi nje chini ya mti wao, si kwa sababu ilimbidi, bali kwa sababu alitaka kufanya hivyo, alikuwa Ibrahimu, alikuwa mtoto wa Mungu, alikuwa amejitenga na mambo ya ulimwengu, naye alikuwa akimwishia Mungu. (Usisahau jambo hilo, Daudi.) Angalieni. . . Huenda msielewe jambo hilo, lakini wale niliozungumza nao walilielewa.

¹⁴⁰ Wakiwa wameketi nje chini ya mti, basi waliwaona watu watatu wakija wamejaa mavumbi nguoni mwao. Basi angalieni walilofanya, tulineni juu yake hivi majuzi usiku, walikuwa ni Malaika watatu, Malaika wawili na Mungu Mwenyewe, nao walikuwa wakienda zao Sodoma, kanisani, kanisa la kimadhehebu kule chini, huko chini katika machafuko, vuguvugu, waliorudi nyuma, wanaodhaniwa kuwa, waliopotelea katika mambo ya ulimwengu, walishuka kule chini pamoja na ulimwengu, kwa hiyo walikuwa wanaenda kuangamia pamoja na ulimwengu.

¹⁴¹ Hivyo ndivyo kanisa litakavyofanya siku hizi, ulimwengu ulio kanisani utaangamia pamoja na ulimwengu. Wale wanaoishi katika dhambi wataangamia pamoja na dhambi, wale wanaomwishia Mungu watafufuka pamoja na Mungu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴² Sasa, hawa Malaika wakiketi pale, sasa, Yeye alisema, “Ibrahimu, nitakuweka tayari kwa ajili ya jambo fulani.” Sasa, Yeye aliwatuma hao watu wengine wawili, nao wakashuka kwenda Sodoma kulihubiri Neno, kama tu vile mhubiri wa kisasa angefanya. Na, lakini Huyu aliyebaki nyuma, ninawatakeni mwangalie matendo Yake. Alimwambia Ibrahimu, akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

¹⁴³ Kisha akasema, “Katika muhula wake nitakurudia, nitakurudia na kukupa mtoto yule sasa.” Sasa, kwa nini Yeye alijiita Mwenyewe, “*Mimi* Ndimi niliyekupa ile ahadi, *Mimi* Ndimi”? Ungewezaje kutilia shaka kwamba ni Mungu? “*Mimi* nilikupa ahadi. *Mimi* nitakurudia. *Mimi* nitakuwa Ndiye nitakayemtoa mtoto huyu.” *Mimi*, kiwakilishi, kiwakilishi nafsi, *Mimi*. “*Mimi* Ndimi niliyelisema. *Mimi* nitakuzuru, kwa muhula wake.”

¹⁴⁴ Na hilo ndilo lililomfanya Sara acheke, akasema, “*Mimi* nikiwa na umri wa miaka mia moja, na bwana wangu ni mkongwe, ingewezekanaje?” Sasa angalieni, ninataka kuwaambia yale aliyowafanyia. Loo, jinsi alivyowaweka tayari kwa ajili yake! Alifanya maandalizi halisi. Kwa hiyo angalieni, Sara akacheke.

¹⁴⁵ Naye Malaika, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, akasema, “Kwa nini Sara akacheke?” Ndipo Sara akatokea na kusema hakucheka. Naye Malaika akamwambia yale aliyosema, yale hakusema kamwe, ila yale aliyowazia moyoni mwake. Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akimtayarisha Ibrahimu kuamini, kumwamini Yeye kwa ajili ya kumpokea mwanawe aliyeahidiwa.

¹⁴⁶ Mungu amefanya nini? Yeye alikuia katika Pentekoste kwa neema Yake, Yeye alikuthibitishia lile agano kwa kukupa tohara, bila masharti. Na sasa Yeye anafanya nini? Yeye anajionyesha Mwenyewe, Mungu yeye yule ndani yako (Unaliona?), yeye yule kwa kujua mawazo ya moyo wako, akikuweka tayari kwa ajili ya kuja kwa Mwanawe aliyeahidiwa, Kristo Mwokozi wetu. Anakutayarisha kwa ajili ya Mwana aliyeahidiwa.

¹⁴⁷ Alikuwa akimwandaa Ibrahimu kwa ajili ya mwana aliyeahidiwa; sasa Yeye anautayarisha Uzao wa Ibrahimu kwa ajili ya Mwana aliyeahidiwa ambaye tunamngojea. Loo, si litakuwa ni jambo tukufu kumwona?

¹⁴⁸ Yeye alifanya nini? Mnakumbuka, ilikuwa mara baada ya hayo, mara tu baada ya kule kutembelewa ndipo mwana

aliwasili, Sodoma ikateketezwa. Hiyo ni kweli, wasomaji wa Biblia? Hiyo ni kweli. Yule mwana aliwasili ambaye Ibrahimu alikuwa amemngojea, ile ahadi.

¹⁴⁹ Kanisa sasa, Uzao wa Ibrahimu, unaninii, unakungojea Kuja kwa Mwana wa Mungu. Na sasa, Yeye amefanya nini? Yeye amekupitisha katika kila moja ya vitu hivyo, kama tu alivyomfanyia Ibrahimu kwa kuthibitishwa kwa lile agano, akakupa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha kama Roho alivyowajalia kutamka, mambo haya yote mbalimbali kama Yeye alivyoahidi, na sasa amewaleta moja kwa moja na kumtuma Roho Wake miongoni mweni, akiwapa upambanuzi wa Kiungu, kabla tu, kuwatayarisha kwa ajili ya Mwana ajaye. Amina. Ndiyo ishara ya mwisho ambayo Kanisa litapokea.

¹⁵⁰ Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Shakarian asubuhi ya leo, akanipigia simu, alikuwa ndio kwanza awe Washington, jinsi ambavyo kila mtu yuko macho kule, hawajui la kufanya, ninii tu—dakika yoyote tu mtu atasimama kubonyeza kitu ambacho kitautupilia mbali ulimwengu katika Umilele, kila—kila oksijeni, haidrojeni itapasuliwa, bahari zitakauka, chochote kile, hakutakuwako na kitu ila kaa litakalosalia duniani, lakini kabla ya jambo hilo kutukia, Kanisa linaenda Nyumbani.

¹⁵¹ Kabla chembe moja ya mvua kunyesha, Nuhu alikuwa ndani ya safina; Lutu alikuwa nje ya Sodoma kabla Yeye hajaweza kuuteketeza huo mji; kanisa litakuwa Utukufuni wakati bomu hilo litakapoachiliwa. Na kama huenda likaachiliwa kabla jua halijatua, usiku wa leo, Kuja kwa Mwana kumekaribia jinsi gani? Natumaini mnaelewa, si mwanadamu, ni Mungu miongoni mwetu.

¹⁵² Kama alivyofanya katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Hajawahi kuwafanyia Mataifa hapo awali maishani mwetu mwote, historia ya Mataifa haijawahi kuona hilo. Tafuta kote katika vitabu na wanahistoria upate kujua, kamwe. Hii ni Nuru ya jioni, Nuru ile ile iliyoangaza asubuhi, ni wakati wa jioni, Naye analiandaa Kanisa kwa ajili ya Mwana wa Mungu ajaye.

¹⁵³ Sasa, angalieni tena, kufanya hivyo ilimbidi kumpa nguvu kuu kabla hajaweza kumpokea mwana huyu. Sasa, itawabidi kuniamini juu ya jambo hili, ama, mkitaka. Nitaweka kando kwa muda kidogo tu.

¹⁵⁴ Biblia ni Barua ya upendo. Mwajua, mwanamke mzuri kuliko wote ulimwenguni kwangu mimi ni Bibi Branham, yeye ndiye mpenzi wangu, ninampenda, ninampenda tu kweli. Sasa, hakuna ushika sheria miongoni mwetu, tunaamini kabisa, tu—tunaamini katika neema, tunaamini katika upendo.

¹⁵⁵ Sasa, ninapokuwa tayari kwenda ng'ambo, simnyoshei mkono na kumshika, na kusema, "Jamani, mpendwa Bibi

Branham, usiwe na waume wowote wengine, usimkonyezee macho mwanamume mwingine yeyote.”

¹⁵⁶ Yeye hanishiki ukosi, na kusema, “Pia, Ndugu yangu mpendwa Branham, usiwe na wake wengine.” Hiyo si ingekuwa ni nyumba? Hivyo ndivyo mnavyojaribu kulifanya kanisa. La, hatufanyi hivyo. Ninampenda, almuradi ninampenda, nitadumu mwaminifu kwake; almuradi ananipenda, itakuwa vivyo hivyo, hilo halitusumbui, la.

¹⁵⁷ Ndipo tunapiga magoti, tunaomba, anamwomba Mungu anisaidie. Yeye anakaa nyumbani kuwatunza watoto, mimi natoka kwenda kumfanyia Bwana kazi. Sijawa nyumbani ila muda kidogo tu katika miaka kumi na mitano. Amegeuka kuwa mweupe kama theluji, akikaa tu, kijana mwanamke, akikaa nyumbani, akikutana na umma, akijaribu kutekeleza sehemu yake. Mwanamke wa kupendeza sana ni mke wangu.

¹⁵⁸ Lakini sasa, tuseme kwa mfano, vipi kama nilikuwa ng’ambo na nikawa mpweke sana, ndipo msichana fulani akasema, “Ndugu Branham, unataka kunipeleka nje kwa gari usiku wa leo, baada ya kanisa?”

¹⁵⁹ Ningesema, “Mimi ni mpweke sana, ninaamini nitafanya hivyo.” Vema, basi nilipoenda nyumbani, ingenibidi kumwambia. Sasa, ninaamini angenisamehe hilo, ninaamini, ninaamini angenisamehe hilo. Lakini, ndugu, ningefia njiani mwangu kabla sijafanya hivyo. Kwa nini? Ninampenda kupita kiasi, na—nampenda. Loo, lingeniua! Nisingeweza kumkabili kwake. Na kama ninampenda mke wangu kiasi hicho, vipi kuhusu Bwana wangu? Paulo alisema, “Vitu vyote ni halali, si vyote vifaavyo.” Mnaona?

¹⁶⁰ Ananiandikia barua, “Mpendwa Billy, nimeketi hapa, usiku wa leo, ndiyo kwanza niwalaze watoto kitandani. Nimefua nguo leo, nimefanya *hivi-na-hivi*. Simu imelia zaidi ya mara mia tatu, watu wanauliza uko wapi. Ninawaza sana juu yako.” Hayo ndiyo anayoandika, lakini, mwajua, ninaweza kusoma moja kwa moja katikati ya mistari na kujua analomaanisha, maana ninampenda.

¹⁶¹ Hivyo ndivyo unavyojua Kitabu hiki cha upendo cha Mungu. Sababu ya kuwa kigumu sana kwa watu, hamumpendi Kristo. Mnasema Hicho—Hicho kinajipinga Chenyewe na yote *haya*, kamwe hampendani na Mwandishi wake, hivyo tu. Ni Barua ya upendo.

¹⁶² Angalieni yale aliyomfanyia Ibrahimu, na kuyaahidia Uzao wake, kabla tu ya kuja kwa mwana, jambo la pili litakalotukia. Mnajua kile alichowafanyia Ibrahimu na Sara? Aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke.

¹⁶³ Loo, unasema, “Sasa, Ndugu Branham, upuuzi huo.” Vema, tutaona.

¹⁶⁴ Sasa, mnaona ya kwamba mara baada ya yule Malaika kukutana naye, kukutana nao kule, walifanya safari ndefu, yapata maili mia tatu, kushuka kwenda Gerari. Hao ni wazee sana kusafiri maili mia tatu, sivyo?

¹⁶⁵ Basi angalieni, sasa Sara alikuwa na umri wa miaka tisini, maskini nyanya, amevaa maskini kofia ndogo, shali ndogo mabegani mwake, fimbo mkononi mwake; huyu hapa Ibrahimu, masharubu makubwa mno, marefu yaking'inia chini, mabega yake yameinama, akitembea namna *hii*.

¹⁶⁶ Loo, unasema, "Sasa, ngoja kidogo, Ndugu Branham. Waliishi . . ." Loo, la, la, la, la. Biblia ilisema walikuwa na umri mkubwa, wote wawili.

¹⁶⁷ Nao wakashuka mpaka Gerari. Sasa, ninataka kuwaonyesha jinsi ingekuwa ni upumbavu kuliamini jinsi watu wanavyoliamini. Basi walipofika kule chini, Abimeleki alikuwa mfalme huko chini katika nchi ya Wafilisti, naye alikuwa akimtafuta mchumba huku kukiwako na hao wasichana wote warembo wa Kifilisti, lakini alipomwona nyanya akiya, alisema, "Huyo ndiye niliyemngojea, huyo ndiye, nilimpenda."

¹⁶⁸ Sasa, likane. Kweli alimpenda Sara na (Hiyo ni kweli?), naye alitaka kumchukua kama mke wake, nyanya, mwenye umri wa miaka mia moja. La, la, ndugu, la, haikuwa hivyo, alikuwa ni msichana mrembo. Alimgeuza akawa msichana, Ibrahimu akawa kijana mwanamume.

¹⁶⁹ Baada ya wao—baada ya kuona ishara hii kuu, ni kitu gani kilichotukia baadaye? Ninaweza kumwona Ibrahimu akisema, "Sara, Mpenzi, makunyanzi hayo yanatoweka kutoka chini ya macho yako mazuri." Ibrahimu anasema . . .

¹⁷⁰ Akajibu, "Ibrahimu, masharubu ya—yako yanageuka kuwa meusi tena, nayo mabega yako yananyoka." Mnaona ilikuwa ni kitu gani? Walikuwa wakiurudia ujana.

¹⁷¹ Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani, kama alikuwa tasa, tumbo lake la uzazi. . . Sasa, kumbukeni, wanawake hawakuvuta sigara siku hizo, kama wanavyofanya siku hizi. Kwa hiyo siku hizi, wakati mwanamke anapovuta sigara, takwimu zinaonyesha ya kwamba mtoto wake mchanga hufa, asilimia themanini kati yao ndani ya miezi kumi na minane kutokana na sumu ya nikotini, inawalazimu kuwalea kwa chupa ya maziwa ya ng'ombe, wanakunywa nikotini. Na kama wakifanya hivyo, wanakuwa wendawazimu kama Ricky na Elvis, na huku nje, mwajua, wakikimbia juu chini, wendawazimu tu. Hivyo ndivyo wamefanya hasa. Mtoto wako akiitwa hivyo, badilisha jina lake. Unaona? Sasa, tukinena kiroho, linamaanisha "Yuda."

¹⁷² Kwa hiyo sasa, angalieni, wakati alipokuwa hapa nje, nao hao hapo, mabega yaliyoinama. Mungu alikuwa amefanya . . . Sasa, angalieni, kama, kabla yeye . . . hajaweza kumpata mtoto huyu . . . Hebu niwaulize jambo fulani. Kabla hajampata mtoto

huyu, ilimbidi Mungu kulirutubisha tumbo lake la uzazi. Hiyo ni kweli? Naye ilimbidi kumfanyia Ibrahimu jambo lile lile.

¹⁷³ Kabla hajampata mtoto huyu, hawakuwa na chupa za afya na za usafi, kwa hiyo yeye, hiyo, hiyo mishipa, mishipa ya maziwa, ilikuwa imebonyea, ingembidi Yeye kufanyiza mishipa mipya ya maziwa, mnajua ninalozungumzia. Na kabla hajafanya hivyo, mwanamke angewezaje, kunradhi, akina dada, sina budi kutoa tamshi hapa, mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja angewezaje kupata utungu na moyo huo? Angekufa moyoni. Mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja, mwenye umri wa miaka arobaini, karibu hivyo, akiingia katika utungu wa kuzaa, hata anakufa, basi mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja, Mungu angempa moyo mpya. Yeye hakumkarabati, alimfanya tu mpya. Amina. Loo, haleluya! Unaona?

¹⁷⁴ Abimeleki akampenda, naye angemwoa. Loo, ninaweza kumwona akioga, na kunyosha miguu yake, baada ya kukariri maombi yake, kisha akaenda kitandani, kasema, “Msichana huyo mrembo wa Kiebrania, nitamwoa, kesho, maana yule ni ndugu yake huko nje, maana alisema hivyo.”

¹⁷⁵ Ndipo Mungu akasema, “Wewe ni kama tu mtu aliyekufa.” Mnaona? “Wewe ni kama tu mtu aliyekufa.” Kasema, “Huyo ni mke wa mtu huyo, nami sitayasikia maombi yako hata kidogo.”

Akasema, “Unajua unyofu wa moyo wangu, mimi ni mtu wa utakatifu.” Kasema, “Unajua unyofu wa moyo wangu.”

¹⁷⁶ Kasema, “Ninaujua, lakini mumewe ni nabii Wangu. Sasa, wewe nenda ukamrudishie mke wake, na umwache akuombe, nitamsikia, bali wewe sitakusikia.” Loo, ndugu! Jinsi ukuu wa Mungu! Jinsi Yeye... Yeye anawajua walio Wake.

¹⁷⁷ Uzao wa Ibrahimu. Mnajua ninachozungumzia? Kanisa, Mungu. Karama zinakujia wapi? Kwa Kanisa la Uzao wa Ibrahimu. Iangalieni leo, iko wapi? Ziko wapi hizi karama za kunena kwa lugha, na karama hizi zingine zote? Ziko wapi? Miongoni mwa Uzao wa Ibrahimu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Alitambua hilo.

¹⁷⁸ Loo, unasema, “Wamefanya mambo mengi mabaya.” Vivyo hivyo na Ibrahimu, alimwita mkewe dada yake. Mtu kufanya hivyo! Mnaona? Naam. Jambo ambalo, haidhuru wamefanya nini, hawajiangalii wenyewe, wanaiangalia Dhabihu yao. Mnaona? Bila shaka.

¹⁷⁹ Sasa angalieni, mara baada ya hayo mvulana mdogo alizaliwa. Mungu alikuwa akionyesha nini? Ishara yake ya kwamba mwana alikuwa yuaja. Basi ni jambo lingine gani alilofanya? Aliwaweka katika hali ya kumpokea huyo mwana.

¹⁸⁰ “Sisi tulio hai, tutakaosalia hata Kuja kwa Bwana hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa maana

parapanda italia nao waliokufa katika Kristo watafufuka. Tutabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na kutwaliwa juu pamoja kumlaki Bwana hewani, na tuwe pamoja na Bwana milele,” huyo Mwana mkuu anayekuja.

¹⁸¹ Mnamwona akiliweka Kanisa Lake tayari? Yeye anafanya nini? Anawaonyesha ishara Yake ya mwisho. Jambo linalofuata ni lipi? Kunyakuliwa, Kunyakuliwa! Mwana anaonekana nasi tunabadilishwa, hatuwezi kwenda kumlaki hewani, Yeye yuko juu sana kwetu, bali tutabadilishwa kama Ibrahimu, baba, alivyobadilishwa, katika kufumba na kufumbua jicho, na kutwaliwa juu pamoja kumlaki Yeye hewani. Huu upatikanao na mauti utavaa kutokupatikana na mauti, huku kuharibika kutavaa kutokuharibika. Ee Mungu, ni saa ya jinsi gani mbele yetu! Jinsi Uzao wa Ibrahimu unavyopaswa kuwa na furaha!

Loo, wakati huo unapotelea wapi? Nami bado sijaanza, nina Maandiko manane ama kumi zaidi hapa ya kurejea, bali itatubidi kuyaachilia.

¹⁸² Kumbukeni, mnalifuata sasa? Mnaona jinsi Mungu alivyofanya maagano hayo, ahadi hizo, na ishara hizo kwa Uzao wa Ibrahimu? Sasa, hiyo karama ya upambanuzi ilienda wapi? Je, ilishuka Sodoma? La, bwana. Miongoni mwa makanisa ya kimadhehebu? La, bwana. Ilikuwa kwa Kanisa teule. Walihubiri Injili, Malaika wawili walishuka wakaenda kule na kuhubiri. Lakini Huyu aliyebaki nyuma kwa Kanisa Teule, lililoitwa litoke, akiwachukua wachache wa Bwana waliodharauliwa. Naye Yesu, Mwenyewe, Mwana wa Mungu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁸³ Mnaweza kunisikia? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaamini hilo? Semeni, “Amina.” [“Amina.”] Ni kitu gani kingine tunachotarajia? Kunyakuliwa, kwenda kumlaki, Mwana ajaye. Itabidi tubadilishwe na kunyakuliwa, huwezi kunyakuliwa jinsi ulivyo sasa, wewe ni mzito kupita kiasi. Loo, lakini, ndugu, siku moja huu unaopatikana na mauti utachukua kutokupatikana na mauti, nasi tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kwa kuwa tutamwona jinsi alivyo.

¹⁸⁴ Loo, ewe Uzao wa Ibrahimu, shikilia ahadi yako, Mpenzi. Dumu nayo, usimruhusu mtu yeyote akunyang’anye hiyo. Kama umetangatanga ukaingia ulimwenguni, nanyi wanawake mmeanza kutenda mambo ya kilimwengu, nanyi wanaume mmefikia kuwaruhusu wafanye hivyo, jioneeni aibu! Unapaswa kuwa boshi wa nyumba, wewe ndiwe mtawala, Biblia ilisema mwanamume atatawala, si mtawala wa kimabavu sasa, mkeka wa sakafuni, Yeye alimfanyia msaidizi, mnaona, mpenzi.

¹⁸⁵ Na jinsi, mambo haya, mnawezaje kuyafanya? Rudini, sivyo? Hivi hamtaniahidi, leo, mtamrudia Mungu? Sina budi kukutana

nanyi wakati fulani, sina budi kukaa pale. Natumaini Yeye ataniruhusu katika siku hiyo, ni—ninajaribu kumtumikia kwa moyo wangu wote.

¹⁸⁶ Sitaki kuwaudhi. Vema, sadaka yenu mliyotoa leo, itasaidia kuwalisha watoto wangu, itanifanyia mambo. Ninawezaje kuwaudhi? Ni—ningekuwa mnafiki duni kufanya hivyo. Lakini sikieni ma—sikieni ma—mahubiri yangu ninayowaambia, mnaona. Lisikieni Neno la Bwana. Mrudie Mungu upesi sana, Mpenzi, rudi upesi sana, useme, “Bwana, ni—ni—ni—nimetangatanga mbali na Wewe, naja nyumbani sasa, Bwana. Ni—nitaachilia yote, na—nataka kuwa binti wa Mfalme; ninataka kuwa mwana wa Mfalme, nataka kusimama mwenye haki. Sijali wengine wao wanasema nini. Mimi . . .”

¹⁸⁷ Ni jambo la mtu binafsi, Yeye hatachukua, hatawachukua tu wa Foursquare pekee, ama hawatachukua tu wa Assemblies pekee, ama wa Umoja pekee, wa Uwili, ama wa Utatu, ama ninii, na kadhalika, Yeye atawachukua walio wakweli moyoni kutoka kwa kila moja lao. Mnaona? Kwa hiyo kwa kuwa si kanisa lako, ama dhehebu, ni jambo la mtu binafsi, kwa hiyo mtafutuni Mungu, mrudieni Yeye. Naam.

¹⁸⁸ Utatawanya Nuru juu ya baadhi yao, labda watachukua wazo la kufanya hivyo. Itawanye Nuru yako, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Hutaki wapotee, ukifanya hivyo, kuna kasoro moyoni mwako. Yesu alikufa kusudi sisi, adui Wake, tuate kuokolewa, bila shaka.

¹⁸⁹ Sasa, karibia sasa, kabla hatujaninii . . . Angalieni, mara baada ya mvulana huyo mdogo kufikia umri wa miaka kumi na miwili . . . Sasa, tuta—tutafunga na kuanzisha mstari wa maombi, sikilizeni tu jambo hili sasa, kwa makini sana. Wakati mvulana huyo mdogo alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, Mungu alisema, “Nitawaonyesha huko Visalia, kwamba kweli ninatimiza ahadi Yangu, maana niliapa nitaitimiza kwa nafsi Yangu.” Aliapa kwake, sio kwa, kwa Ibrahimu pekee, bali kwa Uzao wa Ibrahimu baada yake, aliapa, kwako, kama tu alivyofanya kwa Ibrahimu, akionyesha lile agano, liko na Ibrahimu na Uzao wake.

¹⁹⁰ Akasema, “Nitawaonyesha ya kwamba ninataka walishikilie Neno Langu. Siku moja nitakuwa na mtumishi anayelitwa William Branham, atakuwa akihubiri kule chini, naye atakuwa na kundi la wagonjwa mbele yake, nami . . . yeye atakuwa katika wakati wa mwisho kabisa, kwa hiyo nitakuwa nikifanya ishara za namna hiyo, kwa hiyo ninataka kuwaonyesha kulishikilia Neno, maana kama lisingalikuwa ni Neno, nisingekuwa nikilithibitisha. Lakini tayari nimewaponya, nao hawana budi kufanya jambo fulani, siwezi kabisa kuchukua, kulimwaga ndani yao, hawana budi kuja kulichukua wenyewe.” Sasa, mnasikia hilo ninyi nyote?

¹⁹¹ Sasa, Yeye alisema, “Ibrahimu, kulihakikisha maradufu, ninataka umpeleke mvulana huyo hapa juu ya mlima nitakaokuonyesha, nami ninataka umwulie huko juu, nitakufanya baba wa mataifa kutoka kwake. Kutoka katika uzao wake nitauinua huo Uzao wa Milele, nami ni—ni—nitakufanya baba wa mataifa, lakini mpeleke mlimani ukamwue.”

¹⁹² Yeye ataninii vipi . . . ? Tayari ana umri wa zaidi ya miaka mia moja na kumi na mitano sasa. Atampelekaje mwanawe juu ya kilima na kumwua, aharibu tumaini pekee alilokuwa nalo? Lakini sasa, ninataka . . . Angalieni, alimchukua mtumishi, asingeweza kumwambia mama, hilo lingekuwa ni jambo baya sana, kumwambia maskini mama yake mrembo, atamchukua mvulana huyo na kumwua.

¹⁹³ Kwa hiyo akakata tu kuni, na kuzitia kwenye gunia, na—na kuziweka mgongoni mwa nyumbu, akawachukua watumishi wawili, akaenda safari ya siku tatu. Sasa, watu hawakuwa na miguu ya petroli siku hizo. Wangeweza kutembea . . . Mimi, nilipokuwa nikishika doria, nilitembea maili thelathini kwa siku kwa muda wa miaka saba, na—nami . . . huo si mwendo mzuri sana wa kutembea. Mtu yeyote mwema angeweza kutembea, angalau kijana kama alivyokuwa wakati huo, angeweza, tuseme, maili ishirini na tano kwa siku, kwa hiyo hiyo ilikuwa maili sabini na tano nyuma kutoka kwenye ustaarabu, ndipo akainua kichwa chake na kuona ninii, macho yake hasa, na kuona mlima kwa mbali.

¹⁹⁴ Akaenda kwenye mlima huu, alipofika kule, akasema, angalieni huu, niko katika Mwanzo 22 sasa, nikifunga, akawaambia wale watumishi waliokuwa na nyumbu, kasema, “Ninyi kaeni hapa, wakati mimi na kijana tukienda kule kuabudu, mimi na kijana tutarudi.” Vipi? Anarudije? Unampandisha huko juu ukamwue.

¹⁹⁵ Ibrahimu, baadaye wakati maelezo ya Kiungu yalipoandikwa juu yake, yeye hakusita katika ahadi za Mungu. La, la. Alijua alikuwa amempokea kama mtu aliyetoka katika wafu, alikuwa karibu kufa, umri wa miaka mia moja, naye alijua Mungu aliweza kumfufua katika wafu.

¹⁹⁶ Akasema, “Mimi na kijana tutarudi.” Ndipo akaweka kuni juu ya mgongo wa Isaka. Ni mfano mkamilifu jinsi gani wa Kristo akiwa na kuni Zake Mwenyewe mgongoni Mwake, madhabahu! Akapanda mlimani, wakafika kule juu, kisha wakatengeneza madhabahu, wakaingia kwenye magugu na vijiti na kuchukua mawe na kuyatandaza, wakatengeneza moto kule juu, naye Ibrahimu alikuwa na moto mkononi mwake, akawasha ninii—akaiwasha moto madhabahu.

¹⁹⁷ Ndipo maskini Isaka akashuku, akasema, “Baba,” akasema, “hii hapa madhabahu, hizi hapa kuni, huu hapa moto, lakini yuko wapi mwana-kondoo wa sadaka?”

¹⁹⁸ Sikilizeni hili, ndugu, hebu iingie ndani kabisa ya moyo wako, Ibrahimu alimwalia na kusema, “Mungu atajipatia Mwenyewe mwana-kondoo.” Loo, jamani! Vipi? Vipi? Hilo ni juu ya Mungu. Wako juu kabisa juu ya mlima huu. Kasema, “Isaka, geuza mgongo wako, Mpenzi,” akaifunga mikono yake.

¹⁹⁹ Basi mwangalieni Isaka, si kurusha mateke na kupaza sauti, bali alijisalimisha kwa mauti kama Mungu, ule Uzao wa kweli wa Ibrahimu alivyojisalimisha, akiwa tayari kupachukua mahali petu, alikuwa amefungwa mikono yake na baba yake mwenyewe, akaifunga miguu yake, akamlaza juu ya madhabahu.

²⁰⁰ Ungeweza kuwazia sasa, moyo wa Ibrahimu? Mvulana wake mdogo mzuri, alizishika hizo nywele ndogo za mawimbi, maskini nywele nyeusi za Kiyahudi, na kuzisukuma nyuma kutoka machoni mwake namna *hiyo*, na kuwazia, “Sijui Mama atafikiria nini sasa?” Akazitupa nyuma, la, asingeweza kuwazia hilo, alikuwa akiwazia yale Baba anayowazia. Akachomoa kisu, akakirudisha maskini kichwa chake nyuma namna *hii*, cha mwanawe mwenyewe, mikono yake ikitetemeka, moyo wake karibu kinywani mwake, akainua mkono wake, utiifu kwa Mungu kuutoa uhai wa mwanawe mwenyewe.

²⁰¹ Ndipo wakati alipokuwa tayari kushusha pigo lake, Roho Mtakatifu akamshika mkono, kasema, “Usiunyoshe mkono wako, Ibrahimu, ninajua sasa ya kwamba unaniamini Mimi.”

²⁰² Na yapata wakati huo, Ibrahimu akasikia kitu fulani, na papo hapo nyuma yake kulikuwa na kondoo dume, si kondoo jike, kondoo dume, kondoo dume amenaswa pembe zake kwenye magugu. Hakuwako dakika chache zilizopita. Alikuwa akifanya nini huko juu? Yuko maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu, kuna simba, mbweha, na kadhalika, mbwa mwitu, wangemla. Na jambo lingine, yeye yuko juu ya mlima ambako hakuna maji. Alifikaje huko? Yehova-yire, Bwana alijitolea Mwenyewe dhabihu. Huyu alikuwa ni Kristo.

²⁰³ Sasa, halikuwa ni ono, halikuwa ni ono, ono halitokwi damu. Ibrahimu akamchukua huyo kondoo dume, akamlaza madhabahuni, akakata koo lake, damu ikamtoka, badala ya mwanawe. Si ono, ilikuwa ni kondoo dume. Kwa nini? Yeye anaweza kuumba, anaweza kujipatia Mwenyewe dhabihu.

²⁰⁴ Utaponaje, mwanangu? Umepita usaidizi wa daktari. Utaponaje, unayeketi hapo, maskini mama, ukitetemeka namna *hiyo*? Utaponaje hapo, mwanangu, uliyelala kwenye hicho, umepooza? Utaponaje, uliyeketi hapa? Utafanyaje hilo? Hilo si lako wewe kuliwazia, Yeye ni Yehova-yire, lakini mbali na hayo, Yeye tayari ametoa Mwana-Kondoo kwa ajili ya ninii yako... Tayari! Yesu ametolewa, Naye tayari amefanya uponyaji, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuukubali, kuliadini. Je, unafanya hivyo? Loo, jamani!

205 Na tuinamishe kichwa chetu kwa muda kidogo tu. Tunapotulia mbele za Mungu, ninawatakeni mwombe. Ni wangapi humu ndani wanaotaka kuikubali hiyo Dhabihu ya Mungu iliyotolewa? Inueni mikono yenu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Loo, jamani, kote jengoni.

206 Baba yetu wa Mbinguni, wanaliamini Neno. Vipi...? Waliinua mkono wao kwa sababu gani? Kwa sababu wanajua ya kwamba Wewe hutimiza Neno Lako. Wasingeweza kufanya hivyo, isipokuwa Wewe ungaliwaambia wafanye hivyo, nao walikuwa watiifu, kama tu Isaka alivyokuwa, tayari kufia mawazo ya kibinafsi, tayari kufa kwa yale daktari angeweza kusema, ama chochote kile. Wao ni watoto wa Ibrahimu, wanaamini, wamezaliwa mara ya pili, wao ni, wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu, pia, wanakuamini Wewe. Wenye dhambi waliinua mikono yao kwamba wanataka kuwa mtoto Wako pia, wapokee, Bwana. Wao ni Wako.

207 Juma hili lote, Bwana, haya ni mahubiri matano ya moja kwa moja yanaingia saa hii sasa, itawadia hivi karibuni, tumewasili. Jambo fulani halina budi kufanya, Bwana, Neno Lako limetokea, ishara Zako zimetokea, Wewe umelithibitisha Neno Lako, sasa ni juu ya watu. Bwana, watakapopitia kwenye mstari huu na kuombewa, jalia wawe na imani, jalia watoke kwenye jukwaa hili wakimsifu tu Mungu, "Kama likitendeka, Mungu ashukuriwe! Lisipotendeka, litatendeka kwa vyovyote vile, Wewe ulisema hivyo. Wewe ndiwe Mungu uliyetoa ahadi, humu jengoni, leo." Tujalie, Baba. Ninaomba, katika Jina la Yesu, mjalie kila mmoja wa hawa kwa Utukufu Wako, na iwe hivyo, Bwana. Amina.

208 Vema. Tuna yapata watu mia tatu ama mia nne wa kuombewa. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba maneno ya mwisho yaliyotoka katika kinywa cha Yesu wakati alipoondoka duniani, maneno ya mwisho aliyosema, Yeye alisema hivi: "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya"? Je, Yeye alisema hilo? Sasa, Yeye aliahidi hilo.

209 Kuna wageni wowote hapa, hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii? Inueni mikono yenu, hamjawahi kuwa katika mmojawapo wa hiyo hapo awali, inua mkono wako. Wapo kadhaa. Huenda ukaniambia basi, "Ndugu Branham, ulinena nasi juu ya Malaika ambaye angekuwa hapa katika siku za mwisho, ambaye angekuwa anaishi katika mwili wa mwanadamu, ingekuwa ni Mungu akiishi katika mwili wa mwanadamu. Sijui lolote kuhusu mambo haya, bali ulisema yatakuwako. Sijawahi kumwona akifanya hivyo kama alivyofanya kule chini kuonyesha ya kwamba tulikuwa Sodoma."

Ni wangapi walio wagonjwa huko nje, hawanijui mimi?

Inueni mikono yenu, mna haja. Inua mkono wako, sijali uko wapi. Iweni na kicho kabisa.

²¹⁰ Kabla tu hatujaitisha mstari wa maombi, katika mstari wa maombi hatutakuwa na upambanuzi, maana hatuwezi, tuna mia tatu ama mia nne wa kupitia hapa, nitawaombea, bali hatutakuwa na upambanuzi. Tutakuwa na mstari wa upambanuzi sasa, kwenu ninyi mlio huko nje kwenye kusanyiko.

²¹¹ Sijui hata mtu mmoja huko nje. Nina ndugu *hapa* jina lake Fred Sothmann; ninaye mmoja jina lake Ndugu Tom; nina mmoja, Ndugu Evans, wako huko nje, mahali fulani. Mko wapi? Mko ibadani leo, ndugu? Wako wapi. . . ? Huko nyuma kabisa, naam, huko nyuma kabisa. Hao tu ndio ninaowajua.

²¹² Ni wangapi wenu ninyi wanaume huko nyuma, ninyi wahudumu hamjawahi kuwa na nafasi ya jambo hili? Siwajui ninyi, ni—ni—nilikutana nanyi kule, lakini hilo, sijui lolote kuwahusu, si magonjwa, wala chochote kile. Hiyo ni kweli.

Sasa, hilo hapo, mwasema, “Ndugu Branham, hilo si ni jambo jasiri?” Naam, bali Yeye aliliahidi, naam, bwana, Yeye aliliahidi.

²¹³ Sasa, hebu tuone kama Roho Mtakatifu, kama atalifanya mara nyingine tena, kabla hamjapitia kwenye mstari huu wa maombi, kusudi mwone upako upo hapa, itakuwa sawa kwenu? Mungu na alijalie. Nitajaribu tu kuona kama Roho Mtakatifu angefanya hivyo.

²¹⁴ Ninataka, kugeuza mgongo wangu kwenye kila sehemu, kote kote nyuma yangu, ambao watatoka katika kila sehemu. Ninataka kuwaulizeni swali: Mnaamini Malaika huyo wa Bwana alisema kweli, ninaweza kufanya hivi kwa Roho wa Mungu? Vema. Sehemu hii kupitia huku, kisha tutapitia huku, halafu kupitia huku, na kuzunguka hivi. Mnaona? Ombeni tu sasa, na mwone. . .

²¹⁵ Sasa, Malaika huyo alikuwa ni nani? Huyo, alikuwa ni Mungu, Ibrahimu alisema Yeye alikuwa ni *Elohimu*.

²¹⁶ Sasa, ombeni tu katika sehemu hii, msemi, “Bwana, mtu huyu hanijui, hajui lolote kunihusu mimi.” Ni wangapi katika sehemu hii kupitia hapa wanaojua ya kwamba siwajui, bali hata hivyo ninyi ni wagonjwa na wahitaji? Inua mkono wako. Vema. Nitageuza mgongo wangu. Ninyi ombeni.

²¹⁷ Sasa, Baba wa Mbinguni, hili silo kuninii, hili si onyesho, hili si kufanya maonyesho, bali hili ni kutimiza ahadi Yako, unajua moyo wangu, unajua kusudi langu, na Wewe unajua nia yangu katika kufanya hivyo, ninajua neema Yako kwa kuniruhusu kufanya hivyo. Nami naomba, Baba, ya kwamba utaruhusu lifanyike tena, ili watu wapate kujua ya kwamba nimewaambia ukweli, Uzao wa Ibrahimu ni warithi pamoja naye wa kila ahadi. Tujalie kupitia Jina la Yesu, na sifa zote zitakuwa Zako, Bwana.

218 Nimewaambia watu waziwazi, nao wanajua mimi ni mmoja tu wa watumishi Wako wanyenyekevu sana, sina elimu, sina uwezo wowote, bali Wewe ulishuka tu nilipokuwa mtoto mchanga wa kiume, na, pale kwenye kitanda cha mtoto, kwa *njia moja ama nyingine* Wewe ulinipa tu karama ndogo nipate kujipumzisha, ndipo Wewe uzungumze. Ee Mungu, hilo na liwe. Nisaidie, Bwana.

219 Nisamehe makosa yangu, makosa maishani kwa kuwa mwanadamu, lakini angalia kusudi la moyo wangu na nia. Nami naomba ya kwamba ni mapenzi Yako, alasiri ya leo, kulidhihirisha tena mbele zetu. Kupitia Jina la Yesu, nitakusifu Wewe, na sisi sote tutakusifu Wewe.

220 Watu watakapopitia kwenye mstari huo, watamjua Mungu yeye yule anayejua mioyo yao anajua hali yao, basi, Bwana, jalia kusiwe na kiti cha magurudumu, ila ambacho kitakuwa kitupu; jalia kusiwe na kitanda cha wagonjwa ila ambacho kitakuwa kitupu; jalia kusiwe na mgonjwa miongoni mwetu, ila yule, labda huenda wasiwe wazima kabisa wakati huo, lakini kama Ibrahimu, wanayo ahadi, wataishikilia, Nawe utalithibitisha, Bwana, daima unalithibitisha, kwa kuwa Wewe ni Mungu. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

221 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwa ajili ya kazi ya Roho Wake.

222 Kuna nguvu mbaya nyuma yangu, ni nyeusi, ya kutisha, ni kifafa, iko juu ya mwanamke, ana kifafa. Jina lake ni Bibi Camel. Simama, kubali uponyaji wako, mwamini Bwana Yesu Kristo, na upate afya.

Unaamini sasa?

223 Kuna mwanamke aliyeketi papa hapa karibu nami, naye ana—anaugua ninii, namna fulani ya ugonjwa wa figo, na ni mawe kwenye figo. Naye anamwombea mtu fulani sasa, ni—ni mume wake, naye ana ugonjwa wa akili. Jina lake ni Bibi Lenz. Simama, na upokee uponyaji wako.

224 Unaamini sasa? Amini. Unaamini ni Malaika yule yule wa Bwana? Sasa, vipi kuhusu kushuka kupitia hapa? Kuna mtu yeyote aliye mgonjwa chini kupitia hapa? Inueni mikono yenu.

225 Yupo mwanamke papa hapa nyuma yangu, ni mwanamke, naye ana uvimbe, uko kwenye mapafu yake. Jina lake ni Bibi Spangler. Simama, Bibi Spangler, na ukubali uponyaji wako.

Sasa mnaamini? Siwajui watu hawa, sijawahi kuwaona.

226 Jambo lingine, sasa angalieni huku, angalieni huku sasa, Bibi spangler, nisaidie, weka mkono wako juu ya mama aliye karibu nawe hapo, ana ugonjwa wa figo na anataka kuponywa. Hiyo ni kweli. Sasa, wewe weka mkono wako juu ya yule aliye karibu nawe, ana ugonjwa wa figo na anataka kuponywa. Sasa,

wewe weka mkono wako juu ya mwanamke aliye mbele yako, mwanamke huyo aliyevaa sweta nyekundu hapo, akimwombea mumewe. Hana budi kwenda hospitalini kwa ajili ya kudhoofika kwa mwili wake, anamwombea mumewe. Unaamini? Basi utapona. Amina.

Mnaamini kwa mioyo yenu yote? Mwaminini Mungu. Msiwe na shaka. "Kama unaweza kuamini!" Unaamini kwa moyo wako wote?

²²⁷ Huko nyuma katika sehemu hii ninamwona msichana mmoja, anaomba kwa ajili ya wokovu wa baba yake. Amini, ewe msichana, utalipokea. Usilie, amini tu.

²²⁸ Kuna mama mwingine anayekuja mbele yangu, yuko nyuma yangu, ana ugonjwa wa ini. Kuna wawili ama watatu pale. Na—naihisi, lakini ninamwona mmoja, jina lake ni Bibi Watham. Amini kwa moyo wako wote, na upokee uponyaji wako.

²²⁹ Yupo mama nyuma yangu anayecheza kinanda, ana ugonjwa fulani mgongoni mwake. Kuna mhudumu nyuma, mwenye ugonjwa wa mgongo, pia. Usiwe na shaka. Unaamini kwa moyo wako wote?

Haya basi. Unamwamini Yeye?

Nampenda, nampenda

Kwani . . .

Liamini kwa moyo wako wote sasa.

. . . alipenda kwanza . . .

²³⁰ Mtaamini hapa chini? Kila mmoja wenu hapa chini kwenye vitanda hivi, mtaamini? Mtaamini huko nje? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Malaika yule yule wa Mungu yupo hapa, leo hii? Inua mkono wako, useme, "Ninaamini." Mnaona jinsi alivyo wa kweli, jinsi alivyo halisi?

²³¹ Sasa ni wangapi wanaoamini kama ungepitia kwenye mstari huu wa maombi, mikono itawekwa juu yako, upate afya? Ni wangapi wanaomwamini mchungaji wenu, wanaamini ya kwamba yeye ni mtu wa Mungu? Inueni mikono yenu. Nitainua mikono yangu, pia, ninaamini ndivyo alivyo, pia. Sasa, nitamwomba: Njoni hapa mnisaidie, kila mmoja wenu. Njoni moja kwa moja hapa jukwaani. Hebu na tufanye mstari wa maombi hapa; njoni upande huu, nusu yenu, baadhi yenu upande ule mwingine.

Wote walio na kadi ya maombi namba A, simameni mje huku, upande huu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] A.

Mtini Kalvari.

²³² Sasa, ninataka kila mtu uinamishe kichwa chako, kila mtu katika maombi, huku mkiimba *Nampenda*, ninataka kushuka na kuwaombea hasa hawa walio kwenye vitanda vya wagonjwa na machela hapa chini, wanaopata nafuu.

Ninawatakeni mwe mkiomba pamoja nami, ninyi nyote ndugu. Nitarudi jukwaani katika dakika moja tu. Kusanyiko lote liwe likiomba ninaposhuka. Uzao wa Ibrahimu ni...Uko tayari kupokea uponyaji wako?

²³³ [Ndugu Billy Paul anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Si wote wako huko nje?) [Ndugu Billy Paul anajibu.] (Vema, nilifikiri labda wangekuwa...Vema...) [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁴ ...?...kututia mafuta sana hata labda hatutajua mahali tulipo. Ninawatakeni mkumbuke ninawapenda. “Kwaheri,” kweni. Mungu awabariki. Natumaini kuwaona tena mara moja. Mpaka nitakapowaona, sikuzote mfuata njia ya kwenda kwake Yeye anayeufanya mwezi uendelee kuangaza usiku, nyota zikiangaza, kurahisisha mwendo. Nikumbukeni wakati mnapozungumza Naye, mwambieni nampenda. Ninataka kuwaona Huko.

Vema. Je, mstari wenu wa maombi uko tayari? Kila mtu inamisha kichwa chako sasa, na uimbe, *Nampenda*, wakati mstari unapopita.

²³⁵ Baba, Mungu, wanakuja. Katika...

²³⁶ Ninyi wahudumu wote pandeni hapo juu na kuwawekea mikono sasa, pandeni hapo juu, ninawatakeni msimame hapo juu na kuwawekea mikono watu hawa sasa, wanapopita, njoni moja kwa moja.

²³⁷ Ee Baba...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Sijawahi kuona mkutano kama huu, Sijawahi kuuona maishani mwangu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?...maishani mwangu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...maishani mwangu. Sijawahi kuhisi imani kubwa namna hiyo katika mstari mmoja wa maombi maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Loo, hilo ndilo tumekuwa tuingojea.

²³⁸ Ninyi mnaopita sasa, piteni mkimsifu Yeye, piteni mkimwamini Yeye. Hiyo ndiyo njia ya kufanya, njoni, mkiamini. Unapopitia hapa, si kwa mtu, pita...Nawe utajua mchungaji wako ana...?...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁹ ...?...kuitisha mstari wa haraka. Na yote ambayo nimewahi kupitia, siamini kuna mkutano mmoja ambao nimewahi kuhisi imani kubwa sana kama ile iliyokuwa papa hapa kwenye mstari huu. Nina hakika tu kama ninavyosimama kwenye jukwaa hili, mtaona, ninyi ndugu, miongoni mwa watu hawa jambo fulani likitukia. Imekuwa ni ninii kuu...

²⁴⁰ Mnajua ni kwa nini? Ni kwa sababu kwamba hawa wachungaji wanaamini; wao ni watumishi wa Mungu. Sababu ya mimi kuwafanya watu hawa kuja hapa na kuomba, ni ili ninyi watu mpate kutambua na kufahamu, mchungaji wenu ana mamlaka yale yale ya kuwaombea ambayo mimi, ama

mtu mwingine yeyote anayo, nao wamewawekea mikono yao, kama nilivyofanya mimi. Kama utakuwa mgonjwa siku za usoni, usingojee mtu fulani aje na huduma fulani maalum. Mnaona kinachotukia mchungaji wenu anapowaombea? Mnaponywa, pia. Mnaona? Kwa hiyo, wao ni watumishi wa Mungu, wao ni watumishi wa Mungu, waliochaguliwa kuwawekea wagonjwa mikono na kuwaombea wagonjwa, kama tu kitu kingine chochote.

²⁴¹ Kama ninyi...Kama nilipata neema machoni penu kama mtumishi wa Mungu, niaminini, mwaminini mchungaji wenu, maana yeye ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, mwaminini. Sasa, anashuka, baadhi ya hawa wachungaji pamoja nami kusaidia kuwaombea watu hawa kwenye viti vya magurudumu, kama baadhi yenu ndugu mtakuja huku jukwaani, mtoke jukwaani pamoja nami kuwaombea. 

61-0226 Yehova-Yire
Fairgrounds Auditorium
Tulare, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org